# *Sisi Tunataka Kumwona Yesu*

Asante, Ndugu Borders.

2 Hebu na tuendelee kusimama, usiku wa leo, kwa muda kidogo tu, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa ajili ya maombi. Sasa, huku tumeinamisha vichwa vyetu, je, kuna haja ambayo ungetaka kufanya ijulikane kwa Mungu? Acha ijulikane kwa mkono ulioinuliwa.

Mungu, jalia kila mmoja wao.

3 Baba yetu wa Mbinguni, tumekuja, usiku wa leo, katika Jina la Mwanao, Bwana Yesu, Yule mpendwa. Tunakuja tukiomba, tukiamini ya kwamba Wewe utatujalia haja ambazo zimeombwa usiku wa leo, kwa sababu tunaamini, Baba, kwamba inatoka kwenye moyo mnyofu, kwamba kweli wana haja, nayo haja hiyo ni kwa ajili ya utukufu Wako. Nasi tunaomba ya kwamba Wewe utawajalia haja zao, kila mmoja wao.

4 Sasa, huu ukiwa ndio usiku wa pili katika ibada, tunakushukuru kwa ajili ya usiku uliopita, kwa ajili ya wale waliojitokeza kumkubali Kristo kama Mwokozi wao, tukiamini ya kwamba kila mmoja aliyekuwa akirudi nyumbani kutoka katika hali ya kurudi nyuma, kwamba ujuzi wao ulifanywa upya. Wanajua, tunajua, ya kwamba Mungu husimama amenyoosha mkono tayari kumpokea mpotevu anaporudi. Na wale waliokuwa wakitafuta ubatizo wa Roho, tunaomba, Mungu, ya kwamba utaijaza mioyo yao kwa wema Wako na rehema na nguvu. Tujalie, Bwana.

5 Sasa, usiku wa leo, tunapoenda kuwaombea wagonjwa, kama ni mapenzi Yako, tunatumaini ya kwamba hakutakuwako na mtu mnyonge miongoni mwetu, usiku wa leo, ibada itakapokwisha. Jalia wale wanaokufa kwa ugonjwa wa moyo waponywe, wale wanaokufa kwa kansa ambayo madaktari wamepambana sana kujaribu kuyaokoa maisha yao, lakini inaonekana kana kwamba hakuna matumaini, lakini Mungu, kuna Zeri katika Gileadi, nasi tunashukuru sana kwamba... kujua hilo, na kushiriki ahadi za Mungu sisi kwa sisi.

6 Tunaomba ya kwamba Wewe utakuja miongoni mwetu, usiku wa leo, kwa imani kuu sana, Bwana, hata kutakuwa na wakati mzuri sana. Nasi tunaomba ya kwamba Wewe utakuwa ha—halisi sana kwa kila mtu usiku wa leo, Bwana, hata tutakapoondoka kwenda nyumbani mwetu tutasema, kama wale waliotoka Emau siku ile, baada ya kufa, kuzikwa, na kufufuka kwa Bwana wetu. Walikuwa wakishangaa barabarani,

"Hivi kweli alifufuka ama hakufufuka?" Lakini alipowaingiza ndani, wakati wa jioni, yapata wakati huu ama baadaye kidogo, milango ilikuwa . . . [Unabii umetolewa—Mh.]

7 Amani Yako na rehema Zako, Ee Mungu, ziwe pamoja nasi na kutusaidia, na kumwokoa kila mmoja, Bwana, anayeteseka. Jalia Roho Mtakatifu afanye kazi kuu ambayo ametumwa kufanya miongoni mwetu, nasi tutainamisha vichwa vyetu katika unyenyekevu na urahisi na kukushukuru na kukusifu. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

8 Ndugu huyu ndiyo kwanza aweke hapa haja kadhaa za maombi, nasi tunatumaini ya kwamba Bwana Mungu atalijalia hili na wengi wa . . . [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Leso, na . . . naam.

9 Sasa, tunaamini katika kuombea leso kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka. Sasa, tunatoa hilo katika Biblia. Siku moja huko Afrika Kusini, ninaamini kimoja cha vitabu, huko nje walivyo navyo, kina picha yake, nilikuwa na magunia kadhaa makubwa yaliyojaa leso, zilizokuwa zimetumwa na watu, ndipo wakasema, "Ndugu Branham ni mshirikina sana, kwa sababu yeye huombea . . . huombea leso." Wala haikuwa ushirikina, ni la Kimaandiko tu. Na sasa, tunatambua ya kwamba—ya kwamba ni . . .

10 Ninaamini ya kwamba Paulo alikuwa wa kimsingi sana, wa Kimaandiko, katika kila kitu alichofanya. Sasa, sote hatuna budi kuamini hilo kwa sababu (kuamini Biblia), Mungu asingemruhusu mtu huyu kuandika Biblia, vile—vile vitabu katika Biblia ambavyo aliandika. Ninaamini Paulo wa Agano Jipya alikuwa kama Musa wa la Kale. Sasa, Paulo alikuwa na—nabii-mmishenari kwa Mataifa. Sasa, tunatumaini ya kwamba, katika jambo hili, ya kwamba watu wataelewa ya kwamba Paulo . . .

11 Sasa mahali ninapowazia ya kwamba alilipata, kwamba . . . Mnajua Eliya, wakati mmoja, yule nabii mkuu wa Bwana, mwanamke Mshunami alimpoteza mtoto wake, na kwa hiyo akamjia Eliya na kumwuliza habari za huyo mtoto, naye akasema, "Chukua fimbo hii," kwa Gehazi, mtumishi wake, "nenda ukaiweke juu ya huyo mtoto." Nami ninaamini ya kwamba hiyo ndiyo . . . ambapo Paulo alipata wazo la kuwekea leso, maana Eliya alijua ya kwamba chochote alichogusa kilibarikiwa, kama tu angeweza kumfanya mwanamke huyo kuamini jambo lilo hilo. Lakini imani ya huyo mwanamke haikuwa katika kile alichogusa; ilikuwa katika huyo nabii.

12 Ndipo tunaona ya kwamba katika wakati wa Paulo walichukua leso na nguo, hao watu, imani kubwa zaidi, waliamini, nao wakaweka leso hizi na nguo juu ya watu, na pepo wachafu wakawatoka, nao wakaponywa.

13 Sasa, tunajua Paulo ameondoka muda mrefu, lakini Roho Mtakatifu angali hapa. Ni ninii. . . Yeye hana upendeleo, Naye huwapa watu kibali miongoni mwa watu, wahudumu, kuamini ya kwamba mtu huyo, kitu fulani kumhusu ambacho kinathibitisha ya kwamba Mungu yuko pamoja na mchungaji huyo, nao wanaamini hilo. Na wote wa watu wote wanaoamini Injili yote, huchukua leso, nguo, na kadhalika kutoka miilini mwao na kuziweka juu ya wagonjwa na wanaoteseka, nao wanapata afya. Nasi bado tuna mafanikio makubwa zaidi na hilo kuliko kitu chochote ambacho. . .

14 Hapa siku moja, maskini mwanamke Mjerumani, ninazituma kwa maelfu, basi akapokea moja, naye akawaalika majirani zake waingie. Hakuwa na mchungaji, kwa hiyo aliwaalika majirani waingie na kuomba, naye akakiri makosa yake yote. Hilo hapo jambo moja unalopaswa kufanya, ni kusahihisha mambo na Mungu, maana mateso yanaweza kuwa juu yenu kwa kusudi hilo, na kwa hiyo, kuwaleta kwa Mungu, basi ungameni dhambi zenu zote. Naye alipofanya hivyo akakiweka juu yake.

15 Alikuwa amelemaa kwa yabisi kavu kwa takriban miaka ishirini, ndipo akasema, "Vema, ewe mzee ibilisi, sasa kazi imefanywa, kwa hiyo ondoka, mimi huyu hapa naja." Akasimama moja kwa moja na kuondoka kwenye hicho kiti cha magurudumu, rahisi tu namna hiyo. Mnaona? Kasema, "Vema, kila kitu kimekamilika sasa, kazi zote zimekwisha, kwa hiyo simama tu na uondoke." Hivyo ndivyo hatuna budi kuliamini, kwa njia hiyo tu, rahisi tu tuwezavyo kuwa.

16 Sisi. . . Watu siku hizi wanaifanya Injili kuwa ngumu sana kwa watu. Mnaona? Hiyo daima imekuwa ndiyo sababu inapita juu ya vichwa vya watu wa kawaida. Nayo Injili ilitumwa kwa ajili ya wote, lakini kwa kawaida watu wa kawaida ndio wanaoisikia. Luka alisema, "Watu wa kawaida walimsikia Yesu kwa furaha," watu wa kawaida.

17 Na kwa hiyo Mungu huifanya rahisi sana, Yeye alisema katika Isaya, "Hata mpumbavu hapaswi kukosea njiani." Kwa hiyo kamwe hatutaki kuifanya gumu; ni rahisi, urahisi wa kuiamini, kuwa tu na imani. Usiondoke kwake, dumu moja kwa moja nayo, ndipo Mungu hushughulikia hayo mengine.

18 Sasa, jana usiku niliwacheleweshа. Nitajaribu, usiku wa leo, kuwaombea wagonjwa, nami nafikiri Billy aliniambia, muda mfupi uliopita, ya kwamba aliwapa watu lundo la kadi za maombi. Sababu ya sisi kufanya hivyo ni kuwaweka kwenye mstari, kwamba ni nani anayeweza kuja na ni nani hawezi, na kila anayepata kadi anaweza, anaweza kuja jukwaani. Lakini mtu yeyote aliyewahi kuwa mkutanoni anajua kuna watano wanaoponywa katika kusanyiko wakati mmoja anaponywa jukwaani. Daima ni kuu zaidi kwenye kusanyiko, imani.

19 Sasa, watu wengi wanakutaka uwawekee mikono, hilo ni sawa kabisa, hayo ni Maandiko. Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono juu ya wagonjwa watapata afya." Sasa, hilo ni—hilo ni Neno la Mungu, kwa hiyo tunaliamini. Sasa, lakini mliona, hiyo kwa namna fulani ilikuwa ni desturi ya Kiyahudi, haikuwa hivyo kwa Mmataifa.

20 Sasa, wakati binti Yairo alipokuwa mahututi, walituma mtu amwite Bwana Yesu, na wakati Yeye...akiwa njiani kwenda kule yule msichana akafa, labda katika safari Yake kutoka pwani ya bahari hadi nyumbani, ndipo mkimbiaji akaja, kasema, "Msimsumbue, tayari amekufa."

21 Basi angalieni yale Yairo aliyosema, yeye alisema, "Binti yangu yu karibu kufa. Lakini njoo uweke mikono Yako juu yake naye atapona. Atapona." Huo ni wa Kiyahudi, maana yeye alikuwa ni mwalimu, rabi.

22 Lakini je, mlimwona yule Mrumi, Mmataifa? Wakati Yesu alipokuja kumponya mtumishi wake, yeye alisema, "Sistahili Wewe uje chini ya paa langu." Kisha kasema, "Ninii tu... Mimi ni mtu mwenye mamlaka," kasema, "Ninamwambia mtu *huyu*, 'Nenda,' naye anaenda; mtu *huyu*, 'Njoo,' naye anakuja." Mnaona, alikuwa akimwambia Yesu kwamba alimtambua Mwenyewe, Kristo, kuwa na mamlaka juu ya magonjwa yote, kama tu alivyokuwa na mamlaka juu ya watu mia moja waliokuwa chini yake. Mnaona? "Mimi pia ni mtu mwenye mamlaka, nami nikimwambia mtu huyu, aliye chini ya mamlaka yangu, 'Njoo,' ama 'Wewe nenda,' naye anafanya hivyo. Nena tu Neno, mtumishi wangu ataishi." Jambo ndilo hilo.

Mliona yale Bwana wetu aliyosema? Aligeuka, akasema, "Sijaona imani kama hiyo katika Israeli." Mnaona? Mnaona?

23 "Nena tu Neno, hivyo tu ndivyo unavyopaswa kufanya," maana alijua ya kwamba kila ugonjwa, na kila mateso, na kila kitu kilikuwa chini ya mamlaka ya Kristo, yote anayopaswa kufanya ni kunena Neno.

Naye akatuma Neno Lake na kuwaponya. Mnaona? Kwa hiyo tunajua ya kwamba tunahitaji Neno Lake. Ni Neno, linalotufanya huru.

24 Sasa, usiku wa leo, kama mnaweka vifungu, ninataka tu kuweka msingi kidogo. Jana usiku, sababu ya kutowaombea wagonjwa jana usiku, jambo la kwanza, sikujua kama waliruhusu kuwaombea wagonjwa kanisani hapa, au la. Nilijua walikuwa nao kanisani, kundi la ndugu walikuwa wakiidhamini, lakini walikuwa nao kanisani, nami ninataka kuwa mwangalifu sana nisije nikafanya jambo lolote linalowaudhi ama kuwazuia. Ninataka tu kufanya jinsi ninavyowazia ndilo jambo sahihi la kufanya. Ndipo basi mimi—ndipo nikawaona wagonjwa wote na wanaoteseka, kisha ndugu mmoja akasema hakika, waliamini.

25 Leo, ilitokea kwamba niligundua kanisa hili la Open Bible kwamba, jamani, marafiki wazuri sana nilio nao katika kanisa hilo; Ndugu Mitchell alikuwa mmoja wao. Usiku mmoja tulikuwa na mkutano katika kanisa la Ndugu Mitchell, naye mkwewe hakuwa na Roho Mtakatifu, sikumjua mkwewe, wala binti yake, naye alikuwa pale, naye alikuwa tasa, hakuwa na watoto. Basi nilipokuwa ningali nikizungumza, Roho Mtakatifu akanena na huyo msichana na kusema, "BWANA ASEMA HIVI, 'Utampata mtoto,' naye mume wako ameketi huko nje, BWANA ASEMA HIVI, 'Yeye anampokea Roho Mtakatifu,'" akampokea Roho Mtakatifu. Usiku huo baada ya ibada, Ndugu Bryant kamwe hakuwa na watoto bado, kwa hiyo wakaanza kumwita, "Babu," miezi tisa, huyu hapa mtoto mchanga.

26 Kwa hiyo, halijashindwa kamwe. Liangalieni tu, linaposema hivyo, ni kamilifu hivyo. Nina umri wa miaka hamsini na mitatu, niliona maono tangu nilipokuwa mvulana mdogo, Sijawahi kuona moja likishindwa, wala haliwezi kushindwa. Mungu hawezi kushindwa, hilo ni jambo moja ambalo Mungu hawezi kufanya, hawezi kushindwa, na kamwe hawezi, kwa sababu Yeye ni Mungu.

27 Na sasa tunataka kusoma Neno fulani, hapa, katika Biblia, maana ninajua ya kwamba maneno yangu ni neno la mwanadamu, *Haya* ni Maneno ya Mungu, kwa hiyo hayawezi kushindwa. Na sasa, usiku wa leo, kwa ajili ya somo dogo la Maandiko ninataka kuchukua sehemu kadhaa. Kwanza, ninataka kusoma kutoka. . .kwa utaratibu tu sasa, njia tu ya kusoma, na ibada ndogo ya kawaida ya kuliwekea msingi.

28 Huo Ujumbe, usipopata kitu hicho, ninii tu. . .hu—huna budi kuwa na imani. Kuna njia moja tu ya kuponywa au kuokolewa, na hiyo ni kwa imani. Hisia zako, hizo hazitakuokoa, mawazo yako ya akili, hayatakuokoa, haina budi kuwa ni imani. Nayo imani haininii, haiwezi, kamwe haitaweza kushindwa wakati kweli unaiamini.

29 Sasa, ni vibaya sana hatuna yapata mwezi mmoja hapa katika jiji hili, katika jumba fulani la mikutano, ambapo kama tukichukua tu jumbe juu ya imani, kuwajenga watu kwenye hiyo, kuwaacha wagonjwa hawa wote kote jengoni humu, wanaoketi hapa, kuwaacha waje, wakeshe usiku baada ya usiku, waone kitakachotukia, kuangalia imani mpaka kitu fulani kitakapotia nanga kweli, ndipo waipate. Wakati ninii. . . imani inapotia nanga, itadumu, haitatikisika kamwe. Hakuna kitu kinachoweza kamwe kuitikisa imani.

30 Ninakuta kwenye mstari wa maombi yapata tisini na tisa kati ya kila mia wanaokuja jukwaani. . .Loo, nimewasikia watu wakisema, "Loo, Ndugu Branham, nina imani yote." Basi wanafanya nini huko juu? Mnaona? Mnaona? Mnaona, wewe. . . ni tumaini badala ya imani. Unaona? Kama ni imani, unajua

jambo fulani, ni hakika tu, kama umeketi hapa, ni hakika zaidi kuliko unavyoketi hapa.

31 Ni hisi ya sita, hisi tano hazitaigusa, ni hisi ya sita. Hisi tano hazitatangaza imani hata kidogo, ni hisi ya sita, na hisi ya sita ndiyo inayotangaza silaha zote za Mungu. Na silaha zote za Mungu si kitu ambacho ninii . . . moja ya zile hisi tano itatangaza. Mnaamini hilo?

32 Angalieni: Imani, upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, upole, subira, ni nani anayeweza kutangaza hayo kwa baadhi ya sayansi zenu? Huwezi kufanya hivyo. Ni imani, hisi ya sita inayotoka na kuitangaza, "Ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana." Huioni, huionji, huigusi, huinusi, wala kuisikia; unaiamini. Hiyo ni kweli.

33 Na sasa, vipi kama nilikuwa nikifa, nawe . . . mkate mmoja ungeyaokoa maisha yangu, nao mkate mmoja unagharimu senti ishirini na tano, nawe ukanipa pesa za kununua mkate mmoja, senti ishirini na tano? Ningeweza tu kufurahia nikiwa na hizo senti ishirini na tano kadiri . . . na kushangilia kama tu kwamba nilikuwa na huo mkate kwenye huu mkono mwingine, kwa sababu nina pesa za kuununulia huo mkate. Na kama una imani, na haidhuru itachukua muda gani jambo hilo kutukia, unao. Hivyo tu. Unaona? Itanunua kile unachoomba.

34 Loo, laiti tungeweza kupata kiasi hicho pale pale, kama mngeweza tu, ninyi, kama mkifahamu tu kiasi hicho. Si imani ya kiakili, bali kutoka moyoni, basi hakuna mtu, chochote mahali popote, kingeweza kamwe kukuondoa kwake. Wakati kitu fulani kimetia nanga, hilo latosha, usingeweza kukana hilo zaidi ya vile ungeweza kukana kwamba wewe ni mwanadamu. Unaona? Ni sehemu iliyo halisi tu. Hatuna budi kuliamini.

35 Sasa, nataka kusema jambo hili, ya kwamba mimi si mponyaji wa Kiungu, watu huniita hivyo, bali mimi siye; hakuna mtu aliye mponyaji. Kama mtu akija na kusema yeye ni mponyaji, hebu mwangalie jamaa huyo, kuna kasoro fulani. Wala mimi si Mwokozi, ningeweza kuwa mwo—mwo—Mwokozi kadiri tu ningeweza kuwa mponyaji, kwa sababu "Yeye," Kristo, "a*li*jeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tu*li*ponywa," ni wakati uliopita.

36 Kila dhambi ulimwenguni ilisamehewa wakati Kristo alipokufa pale Kalvari. Mnaamini hilo? Kuna upatanisho wa Damu madhabahuni kwa—kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, bali kamwe haitakufaa kitu mpaka uikubali na kuikiri. Wala kamwe hawezi kulishughulikia mpaka kwanza useme, na ulikubali kwa imani, basi Yeye ni Kuhani Mkuu kutuombea tunapokiri. Mnaona, Yeye hawezi kusogea, Yeye—Yeye amefungwa, hakuna kitu anachoweza kufanya, mpaka kwanza ulikubali na kulikiri na kuliamini kutoka moyoni

mwako, ndipo linamgusa Yeye, na ndipo Yeye anaweza kwenda kulifanyia kazi na kukuombea. Haya basi.

37 Kwa hiyo basi, mtu fulani alisema, "Nina uponyaji mikononi mwangu. Nina uponyaji. . . " Loo, vema, kama uko mkononi mwako, basi Kalvari ilipatwa na nini? Ni nini kilichofanyikia Damu ya Bwana Yesu? Kama kupaka mafuta, ama—ama damu, ama moshi, moto, chochote kile, ni uponyaji, basi Kalvari ilipatwa na nini? Ni nini kilichofanyikia Damu ya Yesu Kristo?

38 Si ajabu watu wamechanganyikiwa sana. Laiti wangeweza tu kusimama kwa dakika moja kutambua ya kwamba kumekuwa na. . .ya kwamba cha bandia hutangaza tu kwamba kuna kitu cha halisi. Lakini watu wananinii tu. . .hawajui waende wapi. Kumekuwa na mengi sana yaliyotangazwa katika Jina la "Roho Mtakatifu," mengi sana yametangazwa katika jina la "uponyaji wa Kiungu," mpaka watu wenye akili timamu, ni vigumu kuwalaumu kwa kuogopa. Lakini kumbuka, ewe rafiki, kwa hakika kama kulivyo na mmoja usio sahihi, hapama budi kuwe na mmoja ulio sahihi.

39 Lakini dhambi ni—ni nini? Ni kutokuamini. Haki ni nini? Imani. Nayo dhambi ni haki tu iliyopotoshwa. Uwongo ni nini? Ni ukweli ulioelezewa vibaya. Uzinzi ni nini? Ni tendo la haki lililowakilishwa kwa njia mbaya.

40 Mnaona, mambo yote. . .Kuna mambo mawili tu, hayo ni kweli na uongo. Wala Shetani si muumba, kuna Muumba mmoja tu, huyo ni Mungu. Shetani hupotosha kile ambacho Mungu ameumba. Lakini maadamu una imani katika Muumba, katika Yeye, Mungu huirudisha mahali pake panapofaa.

41 Vipi kama kulikuweko na ubua wa mahindi ukikua huku umewekelewa kipande kimoja juu yake? Ungekua umepinda. Kiokote, uondoe kila kizuizi kinachozuia huo, na ninii—na jua, ambacho unachomoza kuelekea, hatimaye utaikuza ubua huo wa mahindi unyooke moja kwa moja tena. Ukimtoa pepo mchafu, ndipo watu wanasema, "Vema, hakuna kitu kilichonipata." U—unakua umenyooka moja kwa moja, kama unaamini hilo, na unajua ya kwamba jambo fulani lilikupata, hakuna kitu cha kukuzuia kujinyoosha tena moja kwa moja tena. Ishikilie tu.

42 Ni kama tu vile jua, jua ni. . .hudhibiti uhai wote wa mimea. J-u-a hudhibiti uhai wote wa mimea. Majira ya kuchipua yanapokuja, mbegu hiyo ndogo hukaa ardhini, huwezi kuificha. Haidhuru, ukiweka jiwe juu yake, itajipenyeza itoke moja kwa moja chini ya hiyo zege, na kuinua kichwa chake juu, na kumsifu Mungu, uhai wake. Hakika. Hiyo ndiyo sababu unaweza kuzika baharini, unaweza kuchoma mwili wako uwe majivu, lakini utaninii, haidhuru wangekufanyia nini, utafufuka tena.

43 Ni wapi—ni wapi ulipo na nyasi nyingi zaidi katika majira ya kuchipua, kama ukiweka ninii. . .zege yako, blo-. . .mawe juu yake? Moja kwa moja ukingoni mwa unjia wako. Kwa nini? Ni

uhai huo wote hapo chini. Wakati jua hilo linapoanza kuangaza chini, ingawa ipo chini ya zege, haina budi kutafuta njia ya kutokea, kuinua kichwa chake juu, na kumsifu Mungu. Kwa hakika tu kama vile jua hilo linavyoanza kuipiga, inatokeza. Hiyo ni kweli.

44 Na hakika tu kama vile M-w-a-n-a, Yeye ambaye huutawala Uzima wote wa Milele, kama likiigusa hiyo Mbegu iliyorutubishwa, iliyochaguliwa tangu zamani, jambo fulani linatukia, inashikilia, na hapo inashikilia pale, inajipenyezea kupitia kila kizuizi kilichopo, hatimaye inainua kichwa Chake juu na kusema, "Mungu asifiwe, nilijua ilikuwa hivyo." Jambo ndilo hilo. Hiyo ni imani. Liamini. Usijifanye tu kuamini, kuwa mwaminio, wa kweli.

45 Hiyo ndiyo sababu ya mimi kutoa wito wangu wa madhabahuni kwanza, jana usiku, kabla hatujaanza mstari wa maombi. Tungeweza kufanya mstari wa maombi jana usiku, lakini tulikuwa na watu madhabahuni, hatuna budi kuweka msingi kwanza.

46 Huna budi kuruka juu na kunyakua kitu fulani, hiyo ndiyo njia ya Marekani ya kufanya mambo, kunyakua kama tumbili akifikia chochote king'aacho. Hebu na turudi, na tuingie kwenye msingi wa Injili, Kristo, na hapo, juu ya Mwamba huo, ujenge imani yako, juu ya Kristo, si juu ya hadithi za uongo za jamaa fulani akija huku, na upuuzi mwingi, na kujichochea. Rudini kwenye Neno hilo, na mdumu hapo kwenye hilo Neno, wala msi— msiliache hilo Neno, endapo ni kinyume cha Neno, achaneni nacho, kama kinaambatana na Neno, aminini.

47 Nalo ni Fundisho la busara, la Biblia, la akili timamu, uponyaji wa Kiungu. Endapo hakuna uponyaji wa Kiungu . . . Ni arabuni ya ufufuo wetu. Nimeona kivuli cha mtu anayekufa kwa kansa ya sarkoma akiwa mzima kabisa. Nimeona watu walikuwa wamekufa, taarifa za daktari zikaandikwa, walikuwa wamekufa kwa saa ishirini na nne na kufufuka tena. Ninaweza kuthibitisha hilo kwa taarifa za daktari. Mnaona? Ninajua ya kwamba ni halisi. Mungu ni Mungu, Yeye hawezi kushindwa. Neno Lake ni kweli, lakini huna budi kuliamini, sio tu kuliwazia, kuliamini.

48 Sasa, muda mwingi sana utapita katika kuzungumza nanyi, hata sitalifikia somo langu. Na sasa tunataka . . . Mkinikuta nikisema jambo lolote, nikifundisha jambo lolote ambalo si la Kimaandiko, unawiwa nami kuniambia habari zake. Naam bwana, halina budi kutoka kwenye Biblia hii. Halina budi kuwa ni ahadi ya Mungu. Halafu tunajua ya kwamba kuna . . .

49 Daktari mmoja aliniambia, wakati mmoja, mtu mzuri, laiti ningalikuwa na wakati, niwasimulie hadithi yake, jinsi alivyoongoka, lakini alisema, "Loo, ninaamini, Billy, kama mtu yeyote angeweza kugusa nguzo ile, *huko* nje, na kuamini, wangepona, wanaoamini."

50 Nikasema, "Daktari, ni nani angeweza kuwa na imani katika kuigusa hiyo nguzo? Imani si hadithi ya kubuni. Haina budi kuwa na msingi juu ya kitu fulani. Ni nini kilicho cha Milele zaidi ya Neno la Mungu?"

51 Kama vile maskini yule jamaa mweusi huko chini kusini, alisema, "Afadhali nisimame juu ya Biblia kuliko kusimama Mbinguni." Bosi wake akamwuliza ni kwa nini. Akasema, "Vema, Biblia ilisema, 'Mbingu na nchi zitapita, Neno Langu halitapita.'" Kwa hiyo kama Mbingu na nchi zimetoweka, yeye angali yupo kwa sababu amesimama juu ya Neno. Na jambo ndilo hilo tu, simama juu ya Neno, Hilo ni kweli, Mungu alilisema. Hakuna kingine, hakuna kitu kingine ulimwenguni kitakachochukua mahali Pake. Hakuna taasisi, hakuna dhehebu, hakuna chochote kinachoweza kuchukua mahali pa Neno la Mungu. Na chochote kinyume Nalo ni uwongo nionavyo mimi.

52 Sasa, hebu na tusome hapa sasa, katika Biblia yetu ya thamani, kutoka katika Yohana Mtakatifu mlango wa 12 na kifungu cha 20. Kisha ninataka kuchukua Waebrania 13:8 kwa kuunga mkono kidogo, na hilo sikuzote ndilo kiini cha huu uamsho. Sasa, katika Yohana Mtakatifu mlango wa 12, kifungu cha 20. . . Sasa, kwa kawaida usiku wa kwanza kabla ya uponyaji, ninaliendea somo hili, na kila wakati hujaribu kuliendea tofauti kidogo.

> *Kulikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda kuabudu kwenye sikukuu:*
>
> *Basi hao walimwendea Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakamwomba, wakisema, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.*
>
> *Filipo akaenda akamwambia Andrea, naye Andrea . . . akamwambia Yesu.*

53 Na katika Waebrania 13:8, Biblia ilisema, katika mlango wa 13 wa Waebrania na ki—kifungu cha 8, ya kwamba:

> *Yesu Kristo yeye yule jana, . . . leo, na hata milele.*

54 Sasa, tunataka kuliendea swali hili. Na sasa, na—na—natumaini sitachukua muda mrefu sana kwa ajili ya maskini watu hawa wanaoteseka wanaoketi hapa kwenye viti vya magurudumu hivi, na vitanda vya wagonjwa, na machela, na—nao wako katika hali mbaya, wamelemaa namna hiyo. Lakini kumbukeni, kwamba wao ni . . . Labda watu hawa wanaweza kuishi maisha ya kawaida wakiwa vilema, lakini huenda kukawa na mtu anayeketi huko nje akiwa na ugonjwa wa moyo wala hajui, huenda ikamlazimu kuupata wake sasa, la sivyo atakufa usiku wa leo. Mnaona? Hatujui. Hebu na tuyaweke wazi na dhahiri Maandiko sana, tukiweza, kwa msaada wa Mungu,

ili tuweze ku—kulisaidia kundi zima kupata . . . waone kile tunachozungumzia.

Sasa, nina Maandiko machache, yaliyoandikwa hapa, ninayotaka kuyarejea, na sasa, ninawatakeni muombe pamoja nami ninapofanya hivyo.

55 Sasa, swali ni . . . Kama mmishenari, nimekuwa na ujuzi wa kukutana na dini za kila namna. Nilikaribishwa, hivi majuzi tu, huko Bombay, India, na dini za aina kumi na saba mbalimbali, na kila mmoja wao alimkana Kristo na Mungu. Mnaona? Hilo ni—hilo ni kundi dogo tu lao. Mnaona? Na kuna kila namna ya miungu, kila namna ya kila kitu. Hiyo ndiyo sababu siwezi . . . Sijui ni kwa nini sisi Marekani, chini ya Mungu mmoja, tukiwa na kanisa chini ya kila kona namna hiyo, hatuwezi kuja pamoja, kuwa na ushirika? Kamwe siwezi kuelewa. Ninaweza kuwaelewa watu hao, mu—mungu tofauti. Na sisi je? Mnaona?

56 Sasa, na kila moja ina wazo lao la kubuni. Lakini kila moja ya hizo, waanzilishi wao walikuwa ni watu walioishi na kufa na kuzikwa na wangali humo. Lakini kuna moja yazo tu iliyo ya kweli, na hiyo ni Ukristo. Kwa kuwa Mwanzilishi wa Ukristo aliishi, akafa, na kufufuka tena, kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, naye amekuwa hai kwa muda wa miaka elfu mbili pamoja nasi, hilo linamfanya yeye yule jana, leo, na hata milele.

57 Sasa, nilisoma kutoka Yohana Mtakatifu. Tutarudi nyuma, mlango wa kwanza wa Yohana Mtakatifu, na kuanza tu kuzungumza juu ya Yesu kwa muda kidogo na kujua habari Zake.

Sasa, kama ningewaambia Wa—Wakatoliki wote hapa, "Je, kanisa lako linaamini ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele?"

"Naam."

58 Walutheri, Wabtisti, Wapentekoste, Church of God, Assembly of God, loo, kila mtu angesema, "Naam, hakika." Vema, kuna tofauti nyingi sana mahali fulani, hapana budi pawe na kasoro ama kitu fulani sahihi mahali fulani, kwangu mimi, lime—limevunjika-vunjika sana. Sasa, sasa, kuna njia moja tu tunayoweza kujua, leo, kama Yeye leo ni kama alivyokuwa jana, ni kutafuta kujua kile alichokuwa jana, kisha ujaribu kama Yeye ni yeye yule leo. Sasa, ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

59 Sasa, Wayunani hawa waliomjia Bwana Yesu, ama, waliomjia Filipo wa Bethsaida, wa—wao wenyewe walikuwa wadadisi. Walikuwa wamesikia habari za Yesu nao walitaka kumwona. Sasa, kuna msemo wa kale, "Ninatoka Missouri, nionyeshe." Sasa, Wayunani hao walikuwa kitu kama hicho, sisi . . . walitaka kumwona.

60 Siamini kuna mtu yeyote aliyepata kusikia Jina Lake la ajabu likitajwa pasipo kutaka kumwona. Ninaamini kama ningesema, usiku wa leo, katika kusanyiko hili, "Ni wangapi wenu wangetaka kumwona Yesu?" Kila mmoja wenu angeinua mkono wake. Hiyo ni kweli? Kila mmoja wetu angetaka kumwona Yeye, kila mahali. Vema basi, Maandiko hayawezi kusema uongo, na kama hawa Wayunani walitimiziwa haja yao ya kumwona, basi kwa nini tusimwone, kama Yeye ni yule yule? Sasa, wazieni tu jambo hilo.

Ninaenda, nichukue wakati wangu. Siwataki mwe na wasiwasi, kaeni tu kimya kwa muda kidogo na kulihoji, tunapozungumza.

61 Sasa, kama Yeye ni yeye yule (Na Mungu anisamehe kwa kutumia neno hilo kutoa hoja, *kama Yeye ni*. Tunajua!), sasa, basi kwa nini tusiweze kumwona kama wao waliweza kumwona? Sasa, Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa, njia pekee tunayoweza kuona kama tuko sahihi au sivyo ni kurudi nyuma na kuona kile alichokuwa jana, na basi Yeye ni yule yule leo, na atakuwa milele.

62 Sasa, kama unajua wakati tamshi hili lilipotolewa, lilitolewa katika Agano Jipya, ilikuwa ni Paulo, tunaamini, akiandika Kitabu cha Waebrania kwa Waebrania, akitenganisha torati na neema. Nasi tunaona hapa ya kwamba alisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana," katika Agano la Kale, "leo, na hata milele," yeye yule. Vema basi, ninaamini ya kwamba katika Agano la Kale bado ilikuwa ni Yesu Kristo, ninaamini ya kwamba Nguzo ya Moto iliyofuata. . .iliwaongoza Israeli nyikani ilikuwa ni Kristo, Biblia ilisema ilikuwa. Mwalimu yeyote anajua ilikuwa ni Malaika wa Agano, ambaye alikuwa ni Kristo.

63 Ndipo Yesu alipokuwa hapa duniani Yeye alisema, "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona. Nilitoka kwa Mungu, nami naenda kwa Mungu." Na baada ya Nguzo hiyo ya Moto kufanyika mwili, katika umbo la mwanadamu, Mwana wa Mungu, alikaa miongoni mwetu, alijidhihirisha Mwenyewe na kumthibitisha Mungu, kwa kuwa Yeye alikuwa ni dhihirisho la Mungu katika mwili, "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake," kisha baada ya kufa Kwake, kuzikwa, kufufuka, na kupaa Sauli wa Tarso alikuwa akienda zake, akishuka kwenda Dameski, kuwakamata hao watu waliokuwa wamefanyika Wapentekoste, na alipokuwa akishuka kwenda zake alibwagwa chini na Nuru kuu, Nguzo ile ile ya Moto, ikarudi kwa Mungu, ilitoka kwa Mungu, ikarudi kwa Mungu, Naye akasema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Akasema, "U nani Wewe, Bwana?"

Akasema, "Mimi ni Yesu," mnaona, "na ni vigumu kwako kuupiga teke mchokoo."

64 Sasa, kurudi nyuma na kutafuta kujua, tunaona ya kwamba . . . tuta—tutaliwekea msingi mkubwa zaidi juma lote, tulifanye dhahiri zaidi. (Lakini si—si—sikuweka saa yangu kengele usiku wa leo, ninaangalia saa ile *pale*.) Kwa hiyo tutajaribu kuiacha namna hiyo.

65 Sasa, Yeye alikuwa katika Agano la Kale Nguzo ya Moto, alikuwa duniani Mwana wa Mungu aliyedhihirishwa, Mungu yeye yule, katika mwili, na sasa Yeye yuko katika umbo la Roho Mtakatifu, Mungu yeye yule katika ofisi tatu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, akijifanya Mwenyewe . . . Hiyo ndiyo sababu Mathayo alisema, "Mbatize katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Ilikuwa ni Ubaba, Uwana, na Roho Mtakatifu, Mungu yeye yule akitumia ofisi tatu mbalimbali, Mungu akijidhili.

66 Mungu, mtakatifu, asingeweza kuja karibu na dhambi. Vema. "Hata m—mnyama akiugusa mlima huo hana budi kuchomwa." Tetemeko lilikuwa kubwa sana hata wakapaza sauti, "Acha Musa anene wala si Mungu," maana dhambi ilikuwa ni mbaya sana. Halafu Mungu, alifanyika mwili miongoni mwetu, akafanya kazi pamoja nasi, Timotheo wa Kwanza 3:16, "Bila shaka siri ya utauwa ni kuu, kwa maana Mungu alidhihirishwa katika mwili," Huyo hapo katika mwili, akijitambulisha Mwenyewe, kutukaribia zaidi kidogo.

67 Sasa, kile . . . Yeye alikufa apate kulikomboa Kanisa na wote waliokuwa ndani Yake. Sasa, Yeye amekuja katika umbo la Roho Mtakatifu, Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, Mungu ndani yetu. Mnaona? Mungu ndani yetu, yeye yule jana, leo, na hata milele, Roho Mtakatifu akitenda kazi, akitekeleza, akimaliza kazi za Kristo, zilizokuwa ndani ya Kristo. Sasa, kumbukeni, yote aliyokuwa Mungu aliyamwaga ndani ya Mwanawe, Yesu Kristo, na yote aliyokuwa Kristo aliyamwaga katika Kanisa Lake, mnaona, yanamfanya Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

68 Sasa, angalieni, hebu tuone Yeye alikuwa ni nani. Sasa, "Hapo mwanzo . . . " wa kwanza . . . Yohana mlango wa kwanza. Tutakaa katika Yohana usiku wa leo. Kesho usiku tutaingilia lingine, masomo na kadhalika, mwandishi mwingine, mahali pengine katika Biblia. Lakini angalieni, sasa, katika maandishi ya Yohana, yanaanza hapa nyuma, "Hapo mwanzo alikuwako Neno."

69 Sasa, neno ni nini? Neno ni wazo lililotamkwa, huna budi kuliwazia kabla hujalitamka. Hiyo ndiyo sababu Yesu aliwaambia Mafarisayo, "Enyi wanafiki, mwawezaje kusema mema, na wakati . . . kuniita mwema . . . ?" na kadhalika, huku akijua mioyoni mwao walikuwa wakimwazia mabaya.

70 Kasema, "Kutoka moyoni . . . ki—ki—kinywa hunena kutoka moyoni." Msipofanya hivyo, basi ni—ni mawazo yenu yakijieleza,

huku nanyi mnasema jambo jingine, basi ni unafiki, halitoki moyoni mwenu.

71 Kwa hiyo "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu," Halikuwa limedhihirishwa bado. "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu," Neno, Kristo ni Neno. Sasa, wakati alipokuja duniani. . . Hapo mwanzo alikuwako Neno, na, Neno wazo, na halafu Neno, mara lilipodhihirishwa katika Edeni, likawa halisi.

72 Mungu hawezi kusema lolote kisha alighairi kamwe. Hiyo ndiyo sababu tunaweka matumaini ye—yetu juu ya Mungu, kwa sababu Mungu akiwa hana kikomo, Yeye hawezi kubadilika. Kama ninaweza kusema jambo fulani leo, kesho huenda nikawazia vinginevyo. Mwaka ujao huenda nikawa mwerevu zaidi, nami ninaweza kuwazia vinginevyo, unaweza; bali si Mungu, kila uamuzi ni mkamilifu. Mungu akiisha kusema jambo lolote, ni la Milele hivyo, haliwezi kubadilishwa kamwe.

73 Na sasa, Mungu. . . Hiyo ndiyo sababu Yesu alikuwa Mwana-Kondoo wa Mungu, aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kwa sababu ilikuwa katika mawazo ya Mungu, basi Neno lilipodhihirishwa, ndipo likafanyika mwili na kukaa miongoni mwetu. Loo, napenda hilo, hilo linanipa tumaini kubwa. Na—na—napenda hilo kwa sababu linatoa hakikisho ya kwamba yule Mungu mkuu asiye na kikomo, tunayemtumikia, alijua mambo yote na alitujua kabla ulimwengu haujapata kuumbwa. Jinsi hilo lilivyo tukufu!

74 Watu wanaogopa. Mnaogopa nini? "Wale aliotangulia kuwajua, aliwaita; wale aliowaita, aliwahesabia haki; wale aliowahesabia haki, tayari amewatukuza." Mnaogopa nini? Mshikilieni tu Mungu kama watoto wadogo, na mshikilie Hilo, na kumwaminini Mungu Baba yenu, Yeye anawapenda, amefanya kila aliloweza kuwakomboa. Nyinyi ni. . .

75 Nayo Biblia ilisema mpinga-Kristo aliwadanganya wote walioishi juu ya nchi, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani, alikuona, akaweka jina lako katika Kitabu Chake, na hiyo ndiyo sababu uko hapa usiku wa leo, kwa sababu umeitikia wito huo. Mungu alikujua tangu zamani na akakuita, nawe ukakubali wito Wake.

76 Sasa, unasema, unaweza. . . Mimi. . . Kila mtu anatafuta wokovu wake mwenyewe kwa hofu na kutetemeka. Natumaini jina langu lilikuwa miongoni mwa hao, lakini kama lilikuwa, jina langu daima liko kwenye Kitabu cha Uzima, liliwekwa mle kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa kwa ajili yangu katika mawazo ya Mungu, Yeye hana kikomo. Huendeshi tu shughuli ovyo ovyo, siendeshi

shughuli zangu namna hiyo, wala wewe usingeendesha zako, Mungu haendeshi Zake. Kristo alikuja kuwakomboa wale ambao Mungu alitangulia kuwaona na kujua tangu zamani kwamba wangemjia. Hivi huna furaha kwamba umekuja?

77 Na sasa, kwa uchaji. Unasema, "Ndugu Branham, niko huko?" Sijui, kama uko Kanisani, uko kule. Na njia noja pekee ya kuingia Kanisani: "Kwa Roho mmoja, sote tumebatizwa kuwa mwili mmoja," kwa Roho Mtakatifu. Hatujiungi Nao. Kujiunga na kanisa ni sawa, lakini nimekuwa na familia ya Branham miaka hamsini na mitatu, wala kamwe hawajaniomba nijiunge na familia hiyo, nilizaliwa ndani yake, kwa hiyo nikawa Branham kwa kuzaliwa. Na hivyo ndivyo mtu anavyokuwa Mkristo, wakati anapozaliwa na Roho Mtakatifu. Na basi kama umezaliwa na Roho Mtakatifu basi utakuwa, kwa njia ya Kristo, ukiwa umekufa katika Kristo unachukua Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, na ni warithi pamoja na Ibrahimu, kulingana na ahadi.

78 Nini, Kanisa linahofu nini? Daima nimeshangaa Wapentekoste wana shida gani. Wao—wao wana—wana imani ya kutosha kuulipua ulimwengu, nao wana imani ya kutosha kwa kila namna ya uponyaji, bali wanaogopa kuitumia. Huyo ni ibilisi. Kama tungeweza kukiondoa hicho kivuli cha weusi chini ya watu, jambo fulani litatukia. Na hilo ndilo kusudi langu hapa.

79 Ninaona watu wawili, matabaka mawili, mojawapo ni la kimsingi. Loo, wanajua mahali walipo kwa kumkubali Kristo, wamewekwa mahali pao ndani Yake, bali hawana imani yoyote. Nami ninaona Wapentekoste, imani chungu zima, bali hawajui wao ni akina nani. Ni kama tu mtu aliye na pesa kwenye benki, hawezi kuandika hundi, na huyo mwingine ana... hana pesa kwenye benki huku anaweza kuandika hundi. Kama ungeweza kuwaleta hao wawili pamoja una kitu fulani. Na kama ningeweza kuwafanya Wapentekoste kutambua ya kwamba wao ni wana na binti za Mungu, wameketi katika ulimwengu wa Roho, sasa hivi, katika Kristo Yesu, ambao Mungu alitangulia kuwajua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ametuchagua kuhubiri... Unahofu nini? Haidhuru ni nini, bembea huko nje; chukua Neno la Mungu na uliamini.

80 Keti, mtoto mchanga, na useme wewe ni Uzao wa Ibrahimu, wakati Ibrahimu alipoviita vitu ambavyo havikuwako kana kwamba vilikuwapo kwa sababu Mungu alisema hivyo. Mtu mwenye umri wa miaka sabini na mitano, mkewe umri wa miaka sitini na mitano, naye akasema watapata mtoto. Unafikiri wanafanya nini? Wanashuka kwa daktari na kusema, "Weka vitu tayari, tutapata mtoto."

Mbona, wanasema, "Huyo mtu ana kichaa." Mtu yeyote anayelichukua Neno la Mungu, ulimwengu huwaiita

wendawazimu.

81 Paulo alisema, "Kwa njia inayoitwa uzushi," kichaa, "hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu." Nina furaha kuungana naye usiku wa leo. Hiyo ni kweli. Paulo, wa kimsingi sana katika Neno, pia.

82 Sasa, angalieni. Yeye alikuwa nini? Chochote alichokuwa, Yeye amekuwa na atakuwa hivyo daima. Sasa, nawatakeni mwone, Yeye alikuwa ni Neno, alikuwa ni wazo la Mungu la Mkombozi lililodhihirishwa. Hivyo ndivyo alivyokuwa. Yeye alikuwa ni Neno. Na katika Waebrania mlango wa 4 na kifungu cha 12, Biblia ilisema kwamba "Neno la Mungu lina nguvu zaidi, ni jepesi, kuliko upanga ukatao kuwili, hata Huyatambua mawazo na...ya moyo." Mungu hata anajua kilicho niani mwako. Sasa, shikilia hilo. "Neno la Mungu lina nguvu zaidi, lina ukali, kuliko upanga ukatao kuwili, na Huyatambuaa mawazo ya moyo." Hilo ni Neno.

Hiyo ndiyo sababu hawangeweza kumwamini Yesu, hawangeweza kumwelewa.

83 Yeye aliwaambia, "Yachunguzeni Maandiko, Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Yachunguzeni Maandiko." Aliwaambia wale makuhani wenye elimu, wasomi, "Ninyi yachunguzeni Maandiko, Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Kwa maneno mengine, "Wao...Ninayadhihirisha Maandiko, ninalifanya Neno la Mungu kuwa halisi. Yachunguzeni Maandiko." Walikuwa na wazo lao wenyewe kuhusu jambo hilo, bali Yeye alikuwa na njia sahihi.

84 Walikuwa na vile Masihi atakavyokuja labda chini kupitia ushoroba wa dhahabu na kupeana mikono na Kayafa, kuhani mkuu, kama Yeye angekuja kwa njia yake. Lakini angalieni jinsi alivyokuja, kamwe hakuja kinyume na Maandiko, alikuja jinsi hasa Maandiko yalivyosema. Akasema, "Yachunguzeni Maandiko, Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Wao... Ninayadhihirisha Maandiko. Na nisipofanya udhihirisho kwa matendo Yangu, basi msiniamini Mimi."

85 Loo, ni tamshi la jinsi gani! Mtu ambaye angeweza kuchukua Neno la Mungu lililoandikwa na kulifanya litimie moja kwa moja mbele zao, na bado, kwa mapokeo yao, walimkataa. Si ajabu, "Njia ni pana, inayoongoza kwenye uharibifu." Kweli. "Mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani." Kristo akisimama pale! Kila mtu anataka kitu ambacho kina madoido, kilicho na mapambo mengi juu yake; Kristo ni unyenyekevu.

86 Hapa si muda mrefu uliopita, mtu *fulani*, rafiki yangu, nilipaswa kwenda Chicago kuhubiri katika mkutano mkuu, na kwa sababu kwenye kanda nilikuwa nimetoa taarifa ya kwamba Hawa hakula matofaa, huyo mtu akanikatalia. Basi alipofanya hivyo, alienda na kumchukua mtu fulani, kasisi mkuu

kutoka kwenye taasisi kubwa ya Chicago, ndipo mtu huyo akaja kuzungumza.

87 Basi alipofanya hivyo, alikuwa ameandika kila kitu katika kitabu, karibu namna *hiyo*. Mahubiri ya kiakili, usingeweza kusikia mazuri zaidi. Lakini alikuta wakati alipolinena, halikuendana na watu wa full Gospel, mawazo hayo ya kiakili. Alipanda kwa kishindo pale kifua mbele, na kuyatupa pale, na hata akawafanyia mzaha na kadhalika. Lakini alipofanya hivyo, alikuta kwamba halikwenda vizuri sana. Kwa hiyo akaona kwamba alikuwa amekosea, akafunga vitabu vyake, akashuka chini huku mabega yake yameinama, akishuka kwa unyenyekevu.

88 Kulikuwako na mtakatifu mmoja mkongwe ameketi pale, pembeni, akamgusa aliyekuwa karibu naye, kasema, "Kama angelipanda juu jinsi alivyoshuka, angelishuka jinsi alivyopanda juu." Kwa hiyo karibu ni sawa.

89 Watu, waliozaliwa na Roho wa Mungu, wanamjua Mungu kwa tukio, nao ni sawa kabisa na Neno. Wanakwambia, "Roho Mtakatifu ni msisimko. Si *hili*, si *lile*." Ni kinyume na Neno, Neno lilisema ni kweli.

90 Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Ahadi hii ni kwa ajili yenu, kwa watoto wenu, wote . . . hao walio mbali, wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Ni kwa yeyote atakaye, na aje.

91 Sasa, angalieni, Yesu angeweza kusimama pale na kusema, "Nisipozitenda kazi ambazo Baba Yangu alisema nitazifanya, basi msiniamini Mimi. Sasa, enendeni mkayachunguze Maandiko. Kama mnashangaa juu ya yale ninayofanya, basi nendeni mkayachunguze Maandiko; kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele; na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Sasa, yaangalieni Maandiko muone ni siku gani mnayoishi."

92 Kasema, "Enyi wanafiki, mnaona jua likitua, mnasema, 'Loo, ni nyekundu na kumetanda, kesho kutakuwa na mvua. Kama ni angavu, kesho kutakuwa na kianga.'" Kasema, "Mnaweza kuutambua uso wa mbingu; lakini ishara ya wakati hamwezi kuitambua. Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi." Sasa, hilo hapo tamshi, lililokuwa likimfanya Mungu yeye yule aliyekuwapo. Akiwa ni Mwana wa Mungu, Yeye alikuwa sawa na Mungu. Kama Biblia ilivyosema, si kitu cha kushikamana nacho maana Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili.

93 Sasa, hiyo . . . Angalieni kile tunachojaribu kuweka sasa, ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Huyu hapa amesimama hapa, nalo Neno la Mungu likitabiri yale yatakayotukia katika siku hiyo, na huyu hapa Yeye amesimama hapa akifanya jambo hilo. Naye akasema, "Yachunguzeni

Maandiko; kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini nikizitenda hizo kazi, nanyi hamwezi kuniamini Mimi, ziaminini hizo kazi."

94 Sasa, angalieni kwa makini sasa. Ni Maandiko gani katika Biblia, Agano la Kale, yaliyomshuhudia Yesu? Yeye alisema, "Maandiko, Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Sasa, kama Yeye alisema ya kwamba...Maandiko yote ni uvuvio, nami ninataka kumwona jamaa huyo anayeniambia yanajipinga Yenyewe. Hayajipingi, yanapatana kikamilifu. "Yamefichwa macho ya wenye hekima na akili," Yesu alisema hivyo, "lakini yatafunuliwa watoto wachanga wanaoweza kujifunza."

95 Kwa hiyo Mafarisayo walikuwa na njia yao kulihusu, lakini huyu hapa Mungu anakuja na njia Yake kulihusu. Mnaona? Mafarisayo wakififikiri ingekuwa *hivi*, Yeye kwa jumla alikuwa nje ya Maandiko kwa mawazo yao, lakini alikuwa kikamilifu katika Maandiko pamoja na njia Yake Mwenyewe ya kuwazia. Kwa hiyo inakubidi kuwa na nia iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yako kuyafahamu Maandiko. Na sasa, "Hayo," Yesu alisema, sasa, "Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi."

96 Sasa, tungeweza kuchukua mwendo wa saa nyingine moja ama mbili, na hata tusiyamalize mambo yaliyoandikwa kumhusu Yesu, kote kote kwa "Yeye ni Uzao wa mwanamke" tangu bustani ya Edeni, Isaya 9:6 ndiyo inayosimuliwa kuhusu kuzaliwa Kwake, na yote kuhusu, "na bikira atachukua mimba," na yote tunayozungumzia.

97 Lakini sasa, kwa kuwa tutapita hilo, Maandiko yanayozungumza kuhusu jinsi Yeye angekuja, nyote mnajua walikosa hilo kwa maili milioni moja, jinsi alivyozaliwa, "Mnyenyekevu, ameketi juu ya mwana-punda akiingia," nao wakakosa kumwona. Anatoka kwenye lile kabila dogo la Yuda na kadhalika, kwa "Bethlehemu ya Yuda, wewe ndiwe mdogo kuliko watawala wote, bali kwako atatoka K—Kristo, Mkombozi." Nao wakashindwa kuona hayo yote.

98 Sasa, lakini tutayakwepa hayo yote na kuyapeleka kwenye Maandiko yaliyoshuhudia kazi Zake, kwa sababu Yeye alisema tu, "Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi nizifanyazo, kwa kuwa zinanishuhudia Mimi." Kwa maneno mengine, "Hamwezi kuamini ya kwamba nilizaliwa na bikira; hamwezi kuamini mambo haya yote yaliyonenwa juu ya Maandiko; kama yote hayo yamewapofusha, wala hamwezi kuyaona, basi jaribuni kwamba kazi nizifanyazo zinanishuhudia Mimi, maana zimeandikwa katika Maandiko." Sasa, mnaona, maana Yeye ni Neno, Naye alikuwa Neno katika Agano la Kale, Yeye ni Neno katika Agano Jipya, na Yeye ni Neno sasa, yeye yule jana, leo, na hata milele, kwa hiyo Yeye hawezi kulibadilisha, Hilo daima ni Neno.

99 Sasa, kazi Zake: Sasa, kama tungefungua, kwenye Agano la Kale, kwa ajili ya usiku wa leo, na kuchukua kitu kimoja kilichoshuhudiwa. . .kilichozishuhudia kazi Zake, tutafungua, nanyi liandikeni, ninyi mnaoliandika, Kumbukumbu la Torati mlango wa 18. Someni tu mlango huo wote, ingekuwa. . . itawafaa kusoma jambo hilo lote, Kumbukumbu la Torati 18. Sasa, tunajua ya kwamba Musa aliiacha Misri, bila kuogopa ghadhabu ya mfalme, naye akamfuata Malaika wa Mungu, maana alisema alihesabu kushutumiwa kwake Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko ule wa Misri.

Sasa, angalieni jambo hilo. Watu ambao Misri iliwaona kama watumwa na wakanyaga matope, Musa aliwaona watoto wa Mungu walioteuliwa.

100 Sasa, yeye alikuwa nabii aliyeitwa. Manabii wanajulikana tangu zamani, wanawekwa Kanisani, kama vile ofisi, zile ofisi tano Kanisani. Kwanza kuna mitume, manabii, waalimu, wachungaji, wainjilisti. Mnaona? Afisi hizo Mungu anazoweka Kanisani. Halafu kuna karama tisa za kiroho katika Kanisa hilo, ambazo ni kunena kwa lugha, unabii, na kadhalika namna hiyo. Tofauti kubwa kati ya manabii, mtu anayetoa unabii, na nabii. Unabii hauna budi kuamuliwa na waamuzi wawili au watatu, nabii anazaliwa nabii na kulelewa nabii. Mnaona? Limekusudiwa tangu zamani na Mungu kwa ajili ya wakati huo.

101 Angalieni, sasa, Musa, akiwa ni huyu ambaye Mungu alikuwa amemwinua, basi wakati wa kuondoka kwake, katika Kumbukumbu la Torati 18 alinena na watoto wa Mungu na kusema kwamba "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi." Musa, yule kiongozi, yule aliyewakomboa Israeli, alinena ya kwamba, "Bwana Mungu wetu atawaondokeshea miongoni mwenu, kati ya ndugu zenu, Nabii kama mimi. Naye Mungu alisema, 'Itakuwa, ya kwamba mtu asiyemwamini Nabii huyo atakatiliwa mbali na watu.'" [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Kwa hiyo hiyo ni kumwinua nabii.

102 Sasa, tunatambua ya kwamba Yeye alikuwa awe ni Mungu-Nabii-mkuu. Ninaamini ya kwamba Daudi, nabii Daudi alikuwa na Roho wa Mungu ndani yake. Alikuwa awe. . . Yesu alikuwa ni Mwana wa Daudi. Mwangalie Daudi, yule mfalme aliyekataliwa, kutoka kwa—kutoka kwa watu wake mwenyewe, alipanda juu ya Mlima wa Mizeituni, kisha akaangalia nyuma na kuulilia huo mji kwa sababu alikuwa amekataliwa. Miaka mia nane kutoka hapo, Mwana wa Daudi, mfalme aliyekataliwa, aliulilia Yerusalemu. Hiyo ilikuwa ni nini? Roho wa Kristo kwa sehemu katika Daudi.

103 Mwangalie Yusufu, alizaliwa miongoni mwa ndugu zake, akachukiwa na ndugu zake, akapendwa na baba yake, akapewa koti la rangi nyingi, kama Kristo kikamilifu, angalieni, aliuzwa kwa karibu vipande thelathini vya fedha, akatupwa shimoni

akidhaniwa amekufa. Katika majaribu yake, mnyweshaji na mchinjaji, mmoja alipotea na huyo mwingine akaokolewa, jambo lile lile, Kristo msalabani.

104 Naye alitolewa kwenye shimo hili, akaenda na kuketi mkono wa kuume wa Farao, wala hakuna mtu angaliweza kumwona Farao bila kupitia kwa Yusufu. Naye Yesu alifufuliwa na kuketi mkono wa kuume wa Mungu, wala hakuna mtu awezaye kuja kwa Baba ila kwa njia ya Mwana. Na wakati Far-. . . Yusufu alipoondoka kwenda mbele. . . tarumbeta ililia mbele zake, na kila goti ilibidi lipigwe, "Yusufu yuaja." Na wakati Yesu atakapoondoka kwenye kile Kiti cha Enzi kurudi duniani, parapanda italia, na kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri.

105 Jinsi tungeweza kupitia kwa manabii, na kuonyesha kwamba huyo alikuwa ni Roho wa Mungu, wa Kristo, katika hao manabii! Mnaamini hilo? Mnaona, yeye alitenda tu, akamwonyesha Kristo, ndipo ikaja katika utimilifu wa Nabii.

106 Mwangalieni Musa, jinsi alivyofichwa kwenye manyasi, kama Kristo, kadhalika, akapelekwa Misri, na, loo, chochote tu, mtoa sheria, na kadhalika. Yeye alimwonyesha tu Kristo. Ndipo Kristo alipokuja, ndani Yake mlikuwamo utimilifu wa Roho huyo. Mnaona? Hiyo ilikuwa, "Utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili ulikuwa katika Kristo." Walikuwa nao kwa kipimo.

107 Jambo lile lile, usiku wa leo, kwa Roho Mtakatifu. Mungu, kwenye siku ya Pentekoste, ile Nguzo ya Moto, ilitawanyika ikawa Ndimi nyingi za Moto, Ndimi zilizogawanyika. Badala ya. . . Mungu alikuwa akijigawa Mwenyewe miongoni mwa watu. Siku hiyo, Mungu alikuwa katika Mtu mmoja, Kristo. Sasa, Yuko katika Kanisa zima, la ulimwengu mzima. Amina.

108 Jamani, hilo linanifanya kujisikia kubarikiwa. . .?. . . Sifa kwa Yehova Mungu! Haleluya! Msiniache niwatishe, mimi si mwendawazimu. Kama ndivyo nilivyo, niacheni tu jinsi nilivyo, ninajisikia vizuri zaidi hivi. Kwa hiyo ninii tu, mimi—mimi . . . Wazieni jambo hilo! Kitu fulani hunifurahisha. Tazama, kwamba kwa neema ya Yesu Kristo nimeokolewa usiku wa leo. Kama akija, inaleta tofauti gani? Tutaenda pamoja Naye. Amina. Inastahili zaidi ya mabilioni yote ya ulimwengu yaliyolundikana huku yamejaa kila kitu, na maisha ya kutosha kuishi miaka milioni mia moja, bado nisingebadilishana mahali na mtu huyo hata kidogo. Kufanywa mwana mwenye mamlaka katika familia ya Mungu, na kuwa mmoja wa watoto Wake, ni majaliwa ya jinsi gani! Nao watu wanakipa kisogo kitu kama hicho.

109 Angalieni, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi. Na itakuwa ya kwamba yeyote asiyemsikia Nabii huyu atakatiliwa mbali na watu." Hilo lilikuwa ni fundisho.

110 Sasa, endeleeni kusoma chini ya mlango wako wa 18 pale, Mungu alisema, "Hivi ndivyo utakavyomjua nabii." Israeli

daima walifundishwa kuwaamini manabii wao. Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli-. . . Neno la Mungu lilimjia nani? Nabii. "Neno la Bwana lilimjia nabii Yeremia." "Neno la Bwana lilimjia . . . " Lilikuwa ni Neno la Bwana. Nasi tunajua ya kwamba Mtu huyu alikuwa ni Neno lote la Mungu. Haleluya! Yeye alikuwa ni Neno.

111 Nao Israeli walifundishwa kuwaamini manabii wao. Sasa, Yeye alisema nini? "Akija miongoni mwenu mtu aliye wa kiroho, ama nabii, Mimi, Bwana, nitajitambulisha Mwenyewe kwake katika maono, nitasema naye kupitia ndoto. Na kama yale nabii huyu asemayo yakitimia, basi msikieni, lakini yasipotimia, basi msimsikie." Vema, hilo ni wazi tu.

112 Hakika, kama akisema jambo hilo na lisitimie, ni kosa. Nabii akija akitabiri, lisitimie, basi angalieni mwone kama litatimia, lisipotimia, basi ni uongo; kama likitimia, ni kweli. Hivyo ndivyo Israeli walivyowajua manabii wao.

113 Miaka mia nne sasa, kwa kuzaliwa kwa Kristo, hakukuwako na manabii; Malaki alikuwa ndiye nabii wa mwisho. Loo, walikuwa na manabii wengi wa uongo, bali ninamaanisha manabii halisi. Siku moja, huko chini kabisa kwenye hori la Bethlehemu, alikuja Mtoto mchanga. Kulikuwa na mamajusi kutoka mashariki, walioifuata ishara Yake, nyota ikawaelekeza Kwake. Kulikuwako na wachungaji ubavuni mwa kilima walioshuka kumwona. Alikua kama mtoto mchanga; alicheza kama mvulana.

114 Siku moja kulikuwa na nabii, aliyetoka nyikani, jina lake Yohana, akasema, "Wakati ulikuwa umewadia, tubuni na mwe tayari." Mtu wa mwituni, mkubwa, loo, na amejaa nywele, kama angekuja mlangoni pako, ungemfukuza. Naye, jamaa aliyejaa nywele, akatoka pale, na kusimama kwenye kingo za Yordani zenye matope, na kusema, "Tubuni, kwa maana Ufalme wa Mbinguni umekaribia." Naye akayakemea hayo madhehebu na kuwaambia mahali pao, naye alikuwa amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo; aliwachukia wanawake watovu wa uadilifu. Kwa nini? Roho ya Eliya ilikuwa juu yake.

115 Eliya aliwakemea, jambo lile lile, huko nje, hao Israeli katika siku hiyo, na kuwaambia kanuni zao zote za imani, na jinsi ambavyo walipendezwa na Mama Taifa wa nchi, kama vile Marekani imefanya, na kutenda kama yeye, na kuvaa kama yeye, na huyo Yezebeli, naye akamwambia habari zake. Sawa. Hakumchezea.

116 Hiyo hapo inakuja tena, katika mfano wa Yohana Mbatizaji, aliyeahidiwa tena katika siku za mwisho kuondoka tena. Malaki 4, sio Malaki 3 wakati Yohana alipokuja, "Mjumbe Wangu mbele Zangu." Mathayo 11:6. Lakini pia, mnaona, wakati huyu Eliya atakapokuja, mara baadaye ulimwengu utateketezwa kwa moto na wenye haki watatembea juu ya majivu ya waovu; huyo hakuwa Yohana.

117 Unamwona, “Atairudisha imani ya watoto iwarudie baba zao.” Na wakati huyu wa kwanza alipokuja, aliirudisha imani ya watoto kwa baba zao. Mnaona? Ule Ujumbe mchanga, pale, ulikuwa ukienda kwa baba zetu. Na leo wangeiacha, na wakati mwingine kutakuja mmoja atakayeingia ghafla, hakuna mtu anayejua anakotoka wala anakoenda, bali ataingia moja kwa moja na kurudisha imani ya asili ya Kipentekoste ambayo wao, yule parare wa Katoliki ya Kirumi na tunutu, waliula huo Mti wa thamani ukawa kisiki. Lakini Mungu alisema, “Nitarudisha, asema Bwana. Itakuwa Nuru wakati wa jioni.” Wakati jua hilo la jioni litakapochomoza, kutakuwako na Mti pale wenye matunda juu yake yapate kuiva. Amina.

118 Mwangalieni tunapomwona. Huyu hapa anakuja siku moja, na akabatizwa na Yohana katika Yordani, Yohana alishuhudia, hakuna mtu mwingine aliyeiona. Hakuna mtu aliyeona, wale Mamajusi...ile nyota waliyoiona Mamajusi, hawakuwa wakiitazamia. Hiyo ni kweli. Yeye huja tu kwa wale anaowatafuta. Yohana alijua, alikuwa akitafuta ishara. Hiyo ndiyo njia, kuwekwa katika Maandiko, nawe utajua ishara ya kweli ya Mungu. Mungu sikuzote husafiri kwa ishara.

119 Angalia, kwamba Mamajusi, walikuwa wakitafuta ishara, kwa sababu walijua Nyota ya Yakobo ilikuwa iinuke. Wanapaswa...Danieli alikuwa mwalimu wao wakati alipokuwa...Mnajua walikotoka, wale Wamedi na Waajemi wa kale. Wangali wanaketi mitaani, watatu katika kundi la namna hiyo, wakisoma. Ndipo walipomwona mgeni huyo wa Mbinguni akitokea, walijua jambo fulani lilikuwa karibu kutukia, nao wakaifuata, mpaka wakamwona Masihi.

120 Basi walipokuja Yerusalemu, wakisema, “Yuko wapi Yeye, aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?” lile kanisa kuu halikujua kitu juu yake; mbaya tu kama ilivyo siku hizi, jambo lile lile. Hilo hapo tena.

121 Tunaona ya kwamba basi Yohana alisema, “Yeye aliyeniambia, kule nyikani, ‘Nenda ukabatize kwa maji,’ alisema, ‘Yule utakayemwona Roho akishuka na kukaa juu Yake, Yeye Ndiye atakayebatiza, Roho Mtakatifu na Moto.’” Naye Yohana alikuwa amesimama pale akingojea ile ishara, akiangalia.

122 Akasema, “Kuna Mtu miongoni mwenu...” Alikuwa na hakika kabisa kwamba litatukia, kasema, “Yupo Mtu miongoni mwenu, sasa hivi, msiyemjua.” Kuna mmoja *hapa*, kama ukiangalia.

123 Baada ya kitambo kidogo akaona ishara juu Yake, akasema, “Ni—nilimwona, nilitambua ishara Yake ya Masihi. Ikaja ile Nuru ya Mungu kama hua, ikishuka juu Yake, Sauti kutoka Mbinguni ikisema, ‘Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa kukaa ndani Yake.’”

124 Huyo hapo akaenda nyikani, alijaribiwa kwa siku arobaini mchana na usiku na Shetani, akifanywa tayari kwa ajili ya huduma Yake. Wakati aliposhuka kupitia Uyahudi, na kutoka huko, akaanza kuwaombea wagonjwa, ishara na maajabu yakaanza kumfuata; watu wakaanza kuamini, baadhi yao walimdhihaki, baadhi yao, ambao Yohana alikuwa amewafanya tayari, wakamtambua.

125 Mmoja wao mle ndani alikuwa ni Andrea, nduguye Simoni Petro. Alikaa usiku kucha pamoja Naye mpaka akashawishika ya kwamba Yeye alikuwa Ndiye Masihi, ndipo akaenda na kumwambia Simoni, akamleta Simoni.

126 Sasa, Simoni . . . wao walikuwa ni wasomi, kama umewahi kusoma maisha yao. Baba yao alikuwa ni mwalimu halisi, Mfarisayo. Sasa, angalieni, tunaingia moja kwa moja kwenye jambo fulani. Msilikose. Ndipo Andrea akamwambia Simoni aje pamoja naye mkutanoni, na mara Simoni alipoenda mbele za Bwana Yesu, ambaye Andrea alikuwa amemwambia alikuwa ndiye Masihi . . .

127 Ninaweza kuwazia nikimsikia Simoni akisema, “Nitamjua, nitajua anavyoonekana. Baba yangu mzee aliniambia siku moja, akasema, ‘Simoni, ninazeeka, nilifikiri ningemwona Masihi, tumetamani kumwona kupitia nyakati mbalimbali, bali ninazeeka sana sasa, labda sitamwona. Lakini ninyi wavulana msidanganyike, kama Yeye akija katika kizazi chenu, kumbukeni kutakuwako na madhehebu mengi ya uongo yatakayopita, lakini kumbukeni, ninyi ni Wayahudi, hamna budi kuliamini Neno la Mungu. Basi sikilizeni, huyo Masihi ajapo, Yeye atakuwa vile hasa Neno lilivyosema angekuwa, Musa, nabii wetu, alisema, “Bwana Mungu wetu atamwinua Nabii miongoni mwetu.” Sasa, imekuwa ni mamia ya miaka hatujapata mmoja. Tuna mambo ya kila namna, bali tunamtazamia.’”

128 Huyu hapa Simoni anakuja, akiingia katika Uwepo wa Bwana Yesu. Naye Yesu, akimtazama, alisema, “Tazama, jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.” Hilo liliondoa ugumu ndani yake. Mnaona, si kwamba tu Yeye alijua alikuwa ni nani, alimjua maskini mzee baba yake mtauwa. Akasema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.”’

129 Naye Petro akatambua, papo hapo, ya kwamba Huyo alikuwa ndiye Nabii yule, kwa sababu alikuwa amesema kweli kabisa. Naye akaanguka miguuni pa Yesu, naye Yesu akamfanya kiongozi wa Kanisa huko Yerusalemu, bila elimu ya kutosha kuandika jina lake mwenyewe. Lakini alikuwa na ufunuo, huo ndio unaohitajika. Sawa. Ilimpendeza Mungu kumweka, kwa sababu alitambua, Kimaandiko, ya kwamba Huyo alikuwa ndiye Masihi.

130 Kulikuwako na mtu aliyesimama hapo jina lake Filipo, lilimchangamsha sana hata . . . Alikuwa akisoma Biblia na

mtu jina lake Nathanaeli. Ni kama maili kumi na tano, ukichunguza, kutoka mahali Yesu alipokuwa akihubiri hadi mahali Nathanaeli alipoishi, labda ilimchukua siku moja kwenda kule. Ndipo akafika kule, naye akamkuta Nathanaeli chini ya mti, akiomba.

131 Ninaweza kumwazia Nathanaeli akisema, "Ee, Yehova, tunakutazamia kuja kwa Masihi. Loo, tuko katika utumwa wa Kirumi. Tutateseka namna hii hata lini? Ee, Yehova mkuu, mtume."

Nami ninaweza kumwazia Filipo amesimama pale, akisema, "Mungu abarikiwe, ngoja mpaka nitakapomwambia. Ngoja tu mpaka nitakapomwambia."

132 Na baada ya kitambo kidogo, aliposema, "Amina," kisha akasimama, hakuzungumza naye juu ya visitu vya machungwa, ama visitu vya ndimu, ama chochote alichokuwa nacho. Alisema, "Njoo, umwone Yule tuliyempata, Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu. Huyu ndiye yule Masihi."

133 Loo, ninaweza kuwazia Filipo akimwambia, "Sasa, ngoja kidogo hapa," ama, Nathanaeli akisema, "Sasa, ngoja, tumekuwa na masomo mengi mno mazuri ya Biblia pamoja kwako kuingia wazimu wa namna hiyo. Sasa, kuna kasoro."

134 Vema, hebu na tuingilie tu mazungumzo yao. Ninaweza kuwasikia baadhi yao wakisema . . . kumsikia Filipo akisema, "Sasa, hebu kidogo, hivi hatufundishwi, kulingana na Maandiko yetu, kwamba ajapo Masihi Yeye atakuwa . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . nabii?"

"Kabisa, Musa alisema hivyo, tunawaamini manabii wetu, Naye atakuwa nabii."

"Je, unamjua yule mzee mvuvi, kule chini, ambaye ulinunua samaki yule kwake, wala asingeweza kutia sahihi risiti?"

"Loo, Simoni? Naam. Loo, hata nilimjua baba yake, Yona, hakika, ninamjua vizuri."

135 "Ndugu yake, Andrea, alimleta mkutanoni jana, na mara alipoenda Mbele ya huyu Yesu wa Nazareti, alimwambia jina lake lilikuwa ni Simoni naye alikuwa ni mwana wa Yona. Vipi kuhusu hilo?"

Ninaweza kumsikia Nathanaeli akisema, "Nitaenda nijionee mwenyewe."

Yeye ana heshima zaidi kuliko Wamarekani wengi, watakaa nyumbani na kukosoa, hawataenda, hata kujaribu kujua. Kwa hiyo wataninii . . .

136 Hawa hapa watakuja, nao wakapiga kona wakizungumza. Ndipo alipokuja Mbele za Yesu, sasa angalieni, na mara alipokuja Mbele za Yesu, Yesu alimwangalia na kusema, "Wewe ni . . . Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!" Huyo

alikuwa ni Yesu jana, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila," Naye akamtazama.

Unasema, "Vema, angalia jinsi alivyokuwa amevalia."

137 La, bwana. Wote walivalia vile vile, watu wa mashariki, wamevaa vazi. Angeweza kuwa Myunani, angeweza kuwa, loo, Mmisri, amevaa kilemba, kila. . .mnaona, Yeye hakumjua kwa mavazi yake. Akasema, "Mwisraeli kweli kweli, ambaye hamna hila ndani yake!" Sio Mwisraeli tu bali, "Yeye ni—yeye ni mtu mwaminifu."

138 Naye akasimama, akamtazama, akasema, "Rabi," ambalo linamaanisha "mwalimu," "ulipata kunijua lini? Hii ni mara yetu ya kwanza kukutana. Unanijuaje?"

Naye Yesu akasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona."

139 Ninaweza kuwazia, kuangalia kote, na hapo alisimama Askofu *Nanii* pale aliyekuwa akisema, "Wa kwanza anayehudhuria mmoja wa mikutano hiyo *atafukuzwa kanisani*." Lakini haikuleta tofauti yoyote, alimwona Masihi wa Kimaandiko, naye akakimbia kule, akaanguka miguuni Pake, na kusema, "Rabi, Wewe ni Mfalme wa Israeli; Wewe ni Mwana wa Mungu." Hivyo ndivyo Yesu alivyojitambulisha Mwenyewe jana, hivyo ndivyo walivyojua Yeye alikuwa.

Mwangalieni Yesu akigeuka, kasema, "Kwa sababu nimekwambia hivi unaamini? Utaona makubwa kuliko haya." Huo ulikuwa ndio utambulisho Wake.

140 Jinsi tungeweza kumwendea kipofu Bartimayo, na kuendelea kwa wengine wengi, wengine wengi, na kuendelea kote!

141 Sasa, kuna matabaka matatu tu. . .jamii za watu duniani. Najua humwamini hilo, ama, sisemi *nyinyi* hamwamini, wengi hawaamini hivyo. Mkutano huu, huu unarekodiwa, unaenda kote ulimwenguni. Kwa hiyo kuna watu wengi ambao hawaamini. Kwa hiyo kuna watu wengi ambao hawaamini. Sababu ya mimi kusema hili hivi na kuzungumza jinsi ninavyozungumza, si *ninyi* hasa, bali hii inaenda kila mahali. Mnaona? Imewekwa katika lugha ishirini na saba mbalimbali. Kwa hiyo watu wasioamini. . .

142 Lakini kuna jamii tatu tu za watu, hizo ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi; na hao walikuwa ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria. Mwangalieni Petro akiwa na zile funguo wakati wa Pentekoste, alishuka akaenda kwa Wasamaria, na kupanda juu, nyumba ya Kornelio, na kutoka hapo imefunguliwa. Mnaona, jamii tatu za watu.

143 Sasa, kulikuwako na jamii mbili zao zikimtazamia Masihi, hao walikuwa ni Wayahudi na Wasamaria. Naye Yesu alikuwa na haja, kupitia Samaria. Angalieni jinsi alivyojitambulisha

Mwenyewe miongoni mwa Wayahudi, akiwa ndiye Nabii ambaye Musa alinena habari zake. Sasa, Yeye anawaendea Wasamaria, akaenda mpaka Sikari akiwa njiani kwenda huko chini Ye—Ye—Yeriko, lakini akazunguka, kwa—kwa Wa—Wasamaria, hawana budi kujua, hawana budi kumtambua.

144 Kwa hiyo akaja kwenye mji huu wa Sikari, na kulikuwako na mandhari ndogo, kisima; bado kipo. Naye akaketi pale chini, amechoka safarini, kisha akawatuma wanafunzi mjini kununua chakula. Basi walipokuwa wameondoka, kulikuwako na mwanamke wa kupendeza aliyejitokeza, alikuwa mwanamke mwenye sifa mbaya, alikuwa na waume watano. Alikuwa nyota maarufu wa sinema wa siku hizi. Lakini alikuwa na waume watano huku akiishi na wa sita, angekuwa sawa kabisa siku hizi.

145 Lakini alitoka mjini kuteka maji; asingeweza kuja pamoja na wanawake waadilifu. Kama umewahi kuwa mashariki, utaona wanawatofautisha, nao wanawali huenda mapema kisimani. Alitoka yapata saa tano. Naye huyu hapa akiweka chini ule mtungi mkubwa, unapaswa. . .ni kitu kikubwa mno chenye shingo ndefu, kulabu juu yake. Nimewaona wakiweka mmoja kichwani mwao, mmoja kwenye nyonga *hii*, na mmoja kwenye nyonga *hii*, na kutembea sawasawa tu, na kuzungumza kama wanawake wawezavyo, mwajua, wala kamwe wasimwage hata tone la maji. Hiyo ni kweli. Watembee moja kwa moja kupitia kule, wangali wanafanya hivyo, hawaninii. . .hawajabadilisha hata kitu kimoja tangu siku hizo.

146 Na kwa hiyo, Yeye akaketi karibu na kisima hiki. Akaweka kulabu ndani winchi ipate kuiteremsha kisimani, naye akaanza kushusha ndoo chini, ndipo akamsikia Mwanamume akisema, "Mwanamke, nipe maji ninywe." Naye akaangalia kule, na hapo ameketi Myahudi mwenye umri wa makamo. Alikuwa tu na miaka thelathini na mitatu, si thelathini na mitatu kabisa, lakini mnakumbuka katika Yohana Mtakatifu 6, walisema alionekana kana kwamba alikuwa na hamsini. Kasema, "Wewe ni mtu asiyezidi umri wa miaka hamsini, nawe unasema umemwona Ibrahimu?"

Akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." Mnaona, hawakutambua jambo hilo. Lakini Yeye alisema. . .Yangu. . .

147 Mtu mwenye umri wa makamo yapata miaka hamsini, alionekana mwenye umri wa miaka hamsini, ameketi karibu na kisima. Naye akasema, "Si kawaida kwenu Wayahudi kuniomba mimi, mwanamke Msamaria, kitu kama hicho. Sisi. . .Kuna ubaguzi hapa, hatuna uhusiano sisi kwa sisi."

148 Akasema, "Lakini mwanamke, kama ungejua ni Nani unayezungumza naye, ungeniomba Mimi maji, nami ningekuletea. . .ningekupa Maji usije hapa kuchota."

Mnaona, kile alichokuwa akifanya, sasa, Yeye alikuwa akiwasiliana na roho ya mwanamke huyo.

149 Sasa, mnakumbuka, katika Yohana Mtakatifu 5:19, Yesu alisema, Mwenyewe, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda.” Ni wangapi wanaojua Maandiko hayo? Amina. Si, “Lile ninalosikia Baba analisema,” “Lile ninalomwona Baba analitenda.” Mnaona? Sawasawa na manabii wote waliomtangulia, wadogo, walivyofanya, kama tu vile Mungu alivyowaambia.

Akasema, “Sifanyi neno mpaka nimwone Baba akilitenda.”

150 Sasa, Baba alikuwa amemtuma hapa juu Samaria, kwa Wasamaria, kuwapa Ushahidi wa Masihi. Wayahudi walikuwa wamempokea, baadhi yao, wengi wao walimkataa, asilimia tisini yao, asilimia tisini na tisa, naam, zaidi ya hao walimkataa. Lakini alipowaonyesha Yeye alikuwa ni Nani, basi ilimbidi kuonyesha Samaria kwamba Yeye alikuwa ni Nani—Yeye alikuwa ni Nani.

Ndipo mwanamke huyu akamwambia, akasema, “Kisima ni kirefu, Nawe huna kitu cha kuchotea.”

Akasema, “Maji nitoayo ni Uzima, yakibubujika.” Alikuwa akifanya nini? Akiwasiliana na roho yake.

151 Wakaanza kuzungumza juu ya mahali pa kuabudia, huko Yerusalemu, Naye akasema, “Baba yetu, Yakobo . . . ” Sasa, yule mwanamke Msamaria alimwita Yakobo baba yake, hicho ndicho kile kisima alichompa Yusufu, bila shaka, kasema, “Alikinywea, akawapa watoto wake, na kadhalika. Nawe unasema Maji haya uliyo nayo Wewe ni makuu kuliko hayo?” na kadhalika, wakizungumza.

Ndipo baada ya kitambo kidogo Yesu akaona tatizo lake, mnajua lilikuwa ni nini, akasema, “Nenda, kamwite mumeo mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

Akasema, “Umesema kweli, kwa kuwa umekuwa na watano; na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.”

152 Sasa angalieni, sasa, Mafarisayo walimwona akifanya hivyo, hao wasomi mashuhuri wa siku hizo, nao wakasema, “Mtu huyu ni Beelzebuli, mpiga ramli.” Na mtu yeyote anajua kwamba kupiga ramli ni kwa ibilisi, ni roho iliyopotoshwa.

153 Naye Yesu akasema, “Mkisema neno dhidi Yangu, nitawasamehe; lakini siku moja Roho Mtakatifu anakuja kufanya hivyo, na neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe.” Mnaona, Dhabihu haikuwa imetolewa wakati huo, imetolewa sasa.

Mwangalie mwanamke huyu. Akasema, “Nenda, kamwite mumeo mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

Akasema, "Umesema vema. Umekuwa na watano; na yule unayeishi naye sasa siye mume wako."

Mwangalieni. Ndugu, yeye alijua zaidi juu ya Mungu kuliko nusu ya wahubiri Marekani, katika hali hiyo. Aisee, hiyo si ni kweli?

154 Akasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii." Hao wengine walisema, "Beelzebuli." Naye akasema, "Naona ya kuwa Wewe ni nabii. Tunajua ya kwamba ajapo Masihi, hivyo ndivyo atakavyofanya." Loo, jamani. Walikuwa na mafundisho bora zaidi. Mwanamke huyo, katika hali hi—hiyo aliliona upesi.

155 Ilikuwa ni kitu gani? Moja ya hizo Mbegu za Uzima, zilizochaguliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Na haidhuru ni wa kidini jinsi gani, kile nilichokuwa nikijaribu, kuwaambia jana usiku, kutakuwako na wengi sana watakaohukumiwa wanaodhani kwamba wao ni watakatifu na watauwa. "Hakuna mtu awezaye kuja, asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Na mara hiyo Nuru ilipomulika kwenye ile Mbegu iliyochaguliwa tangu zamani pale, upesi ikawa Hai.

156 Hao wengine wote walikuwa *wamefundishwa Maandiko* na kufundishwa *hili*, *lile*, na *linginelo*, bali yeye alijua, akasema, "Bwana, najua ajapo Masihi, Yeye atatuambia mambo haya."

Akasema, "Mimi ninayesema nawe, Ndiye."

157 Huyo akaingia mjini, hakuhitaji kitu kingine chochote. Akakimbia mjini na kusema, "Njoni mwone Mtu, aliyeniambia mambo niliyofanya. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi." Nayo Biblia ilisema ya kwamba watu wa mji huo walimwamini Yesu kwa sababu ya ushuhuda wa yule mwanamke. Walijua huyo angekuwa ndiye Masihi. Kama huyo alikuwa ni Yeye jana, itabidi iwe ni Yeye leo. Hiyo ni kweli?

158 Sasa, kumbukeni, Mungu anapofanya uamuzi, hawezi kuubadilisha. Hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe kila wakati, hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe kwa Wayahudi, hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe kwa Wasamaria.

159 Sasa, sisi Mataifa, hakuna hata wakati mmoja katika Maandiko ambapo jambo hilo liliwahi kutendewa Mmataifa. La bwana. Kwa nini? Hawakuwa wakimtazamia Masihi yeyote. Tulikuwa na rungu mgongoni mwetu na tukiabudu sanamu siku hizo, sisi Waanglo-Sakson.

160 Lakini angalieni, Yesu alitabiri ya kwamba Roho Mtakatifu angekuja na kufanya jambo lile lile. Sasa, katika kufunga, ningependa kusema jambo hili. Kama vile Ibrahimu. . .Nasi, tukiwa ndani ya Kristo, tunachukua Uzao wa Ibrahimu. Sasa, msilikose.

161 Angalieni, Ibrahimu, ilipofikia wakati wa utengano, yeye na Lutu, Lutu alishuka kwenda Sodoma. Ndipo ikafikia mahali hapa pale, ambapo Mungu alikuwa akitaka kujidhihirisha Mwenyewe. Basi siku moja Ibrahimu, akiketi katika mlango wa hema lake...Aliwakilisha Kanisa la kiroho. Sasa, kuna matabaka matatu ya watu: asiyeamini, anayejifanya mwaminio, na mwaminio. Sasa, asiyeamini alikuwa ni Msodoma; anayejifanya mwaminio alikuwa ni Lutu, kanisa la kawaida, kanisa la kimadhehebu; na ninii...Ibrahimu aliwakilisha Kanisa lililoteuliwa, lililoitwa litoke, lililotengwa, kwanza kabisa hakuwa Sodoma. Loo, jamani. Angalieni, Malaika huyo kamwe hakwenda kwenye kanisa hilo lingine, alikuja kwa Kanisa teule.

162 Hao watatu walikuja, basi angalieni, wakati walipokuja, Ibrahimu alitoka nje na kusema, "Bwana wangu, njoo huku, keti chini," huku ameketi kwenye mlango wa hema lake. Kulikuwa na kitu fulani kuhusu hao Watu, Walikuwa Wageni, mavumbi kwenye nguo Zao, ila jambo ni kwamba, ilikuwa ni Mungu Mwenyewe na Malaika wawili. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Ibrahimu alimwita, "Bwana, Elohimu." Hiyo ni kweli. Bwana Mungu, Yehova, Ajitoshelezaye kwa Yote. Ndipo akapanda, Wakaketi chini, Nao wakazungumza na Ibrahimu.

163 Ndipo wawili kati Yao wakaamka na kushuka kwenda Sodoma. Naye Ibrahimu akaitetea Sodoma, kama angeweza kupata hamsini, kama angeweza kupata ishirini, na kuendelea mpaka, angeweza kupata kumi, Naye aliahidi kuwaokoa kwa ajili ya kumi.

164 Angalieni, huko chini Sodoma walienda wajumbe wawili, bila kufanya ishara zozote na maajabu, Billy Graham wa kisasa, jambo pekee walilofanya lilikuwa ni kuwapofusha, na kuhubiri Injili kunampofusha asiyeamini. Angalieni, naye...walihubiri Injili na kumwita Lutu, naye mkewe akageuka kuangalia nyuma. Tunaijua hiyo hadithi.

165 Lakini Yule aliyekaa pamoja na Ibrahimu, hebu mwangalieni. Alikuwa ameketi huku ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, ndipo akasema, "Wapi...?" Sasa, kumbukeni, alikuwa Abramu mpaka siku iliyotangulia, naye mke alikuwa S-a-r-a-i siku iliyotangulia, lakini sasa, ni S-a-r-a, naye ni A-b-e-r-h-a-m. Akasema, "Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?" S-a-r-a.

Kasema, "Yuko hemani nyuma Yako."

Naye akasema, "Nitakurudia kulingana na wakati wa uhai."

166 Alijuaje alikuwa ameoa? Alijuaje alikuwa na mke, na alijuaje jina lake lilikuwa Sara? Lakini mnaona, "*Mimi*," "Nitakurudia," kulingana na ahadi aliyokuwa ametoa. *Mimi* ni kiwakilishi nafsi. Ilikuwa ni Mungu. Mnaona? Na—Naye akasema, "...wakati wa uhai, wa Sara, itakuwa...atampata mtoto sasa," alikuwa kwenye umri wa miaka mia moja kabisa.

167 Naye Sara, kifichifichi, akacheka, huku Malaika ameketi hapo nje, huku amempa kisogo, kasema, "Kwa nini Sara akacheka, akisema moyoni mwake, 'Mambo haya hayawezekani'?" Hiyo ilikuwa telepathia ya namna gani? Basi hatimaye, huyo Mtu akatoa ishara.

168 Naye Yesu akasema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu."

169 Si ni ajabu, wanaye mtu, wakati pekee katika historia yote ya ulimwengu, huko nje miongoni mwa makanisa ya kimadhehebu, mwenye jina kama la Ibrahimu? A-b-e-r-h-a-m, G-r-a-h-a-m. Ajabu, sivyo? Kanisa la kawaida linatembelewa.

170 Mungu anajaribu kuonyesha nini? Alifanya nini huko? Huyo alikuwa ni Mungu katika mwili wa nyama, ikionyesha ya kwamba Mungu atakuwa katika Kanisa Lake katika siku za mwisho, katika mwili wa nyama, mwili wa wanadamu, katika mwili Wake, na atadhihirisha jambo lile lile. Kwa sababu, kama Wayahudi walikuwa na hiyo. . .Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho waliyopata Wayahudi. Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho aliyopata Ibrahimu kabla ya Moto kushuka, na hii hapa, kufikia wakati uo huo leo.

171 Kama Yesu Kristo amekuja Kanisani kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kunena kwa lugha, na kuwaponya wagonjwa, na kufanya miujiza, ambalo ni jambo lile lile alilomfanyia Ibrahimu safarini, basi hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho kabla ya ule Moto; ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho kabla Mungu hajawaacha Wayahudi.

172 Hii hapa, basi Mataifa hawana budi kupata jambo lile lile, hilo ni Kanisa teule na kanisa la kawaida. Huyo hapo huko nje, na huyu hapa Roho Mtakatifu hapa usiku wa leo, Yesu Kristo yeye yule aliyekuwako jana, leo, na hata milele, kufanya jambo lile lile. Yeye ni Kristo yeye yule, Yeye hawezi kushindwa, Yeye ni Kristo. "Sisi tunataka kumwona Yesu."

173 Kama ningetoka nikaenda mtaani usiku wa leo, na nikamwona mtu, na kumleta hapa ndani, aliye na makovu ya misumari mikononi mwake, na alama usoni mwake *hapa*, na damu ikitiririka kutoka kwenye kovu la msumari, mnafiki yeyote angeweza kufanya hivyo. Lakini Uzima. . .Mungu aliufufua mwili wa Yesu Kristo, nao umeketi mkono Wake wa kuume. Mnaamini hilo? Hiyo ni. . . "Yeye ni Kuhani Mkuu anayeketi huko apate kutuombea tunapokiri." Yeye ni Kuhani Mkuu wa Mungu sasa.

174 Lakini Uhai uliokuwa ndani Yake, Roho aliyekuwa ndani Yake, yuko hapa chini, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Kwa nini Yeye angeweza kuwaambia kile walichokuwa wanawazia, kile walichokuwa wakifanya, kwamba wao walikuwa ni kina nani? Kwa sababu

Yeye alikuwa Neno, "Neno la Mungu," Waebrania 4 ilisema, "ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na Huyatambua mawazo ya moyo." Halafu basi, kama Neno hili. . .imani imeingia katika Neno hili, naye Mungu ameliweka Kanisa Lake katika utaratibu, Neno hilo linakuwa kitu kile kile. Hilo linamfanya Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, kitu kile kile. Mnaamini hilo? Nawapa changamoto kuliamini. Muda unaenda, ninaendelea tu kuzungumza. Nawapa changamoto kuamini hilo kuwa ni kweli.

175 "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Ingekuwa nini zaidi, kama mtu angeingia humu, amejaa damu, na makovu ya misumari, na kadhalika? Yesu, atakapokuja, kila jicho litamwona, kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri wakati mwili wa Yesu utakaporudi. Ninaamini katika kuja Kwake halisi, mwili wa kawaida, akishuka kutoka Mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya Malaika Mkuu, parapanda ya Mungu. Waliokufa katika Kristo watafufuka. Lakini Roho Wake yuko hapa pamoja nasi.

176 Na wakati Kanisa, kama vile piramidi, linapofikia ma— mahali, vivyo hivyo na Kanisa katika siku za Luther, siku za Wesley, siku za Pentekoste. Na sasa kabla tu ya lile Jiwe la Kichwa kulifunika, Kanisa hilo halina budi kuchongoka kikamilifu sana, mpaka huduma ile ile aliyoifanya hapa, Roho Wake yule yule, ametamalaki sana, atauingiza mwili uo huo moja kwa moja ndani Yake, na kukifufua kitu hicho chote. Hiyo ni kweli kabisa. Amina. Utukufu kwa Mungu.

177 Hebu angalia upande wa nyuma wa dola yako ya Marekani, upande mmoja inasema "Muhuri wa Marekani," tai aliyeshika vitu mkononi mwake. Kwa nini waliweka muhuri wa Misri na kusema, "Muhuri Mkuu," upande huo mwingine? Si fundisho la piramidi, huo ni upuuzi. Ninazungumza juu ya jambo fulani wanalosema.

178 Ni kama tu vile, kwa nini mwanamke, kila wakati anapoolewa, hufunika uso wake kwa shela? Anamjia mumewe, kichwa, kama tu Rebeka alivyofanya. Aliweka shela juu ya uso wake kukutana na Isaka. Hana kichwa tena, Isaka ndiye kichwa chake. Nalo Kanisa linapaswa kujitiisha sana kwa Neno la Mungu, hata linaufunika uso Wake Lenyewe, halina kichwa. Ni. . .Tabia ya mwanamke ni kujisalimisha kwa mwanamume. Na hivyo ndivyo Kanisa linavyopaswa kuwa likifanya, likijisalimisha kwa Kristo, kwa Neno Lake, kwa Fundisho Lake, kwa kanuni Zake. Halijiwazii Lenyewe. Halina kichwa, Kristo ndiye Kichwa Chake, si kundi fulani la kikanisa, bali Kristo ndiye Kichwa Chake, Neno, "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu." Haleluya! "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele," dhihirisho lile lile la Neno. Mnaamini hilo? Na tuombe.

179 Baba wa Mbinguni, kuna jambo moja ambalo watumishi

Wako wanawajibika kwalo, kulihubiri Neno. Hivyo tu ndivyo tunavyoweza kufanya, ni kuhubiri tu Neno. "Nyingine huanguka kando ya njia," wengine watasimama na kuondoka, wengine wataketi na kushangaa; wengine watalipokea, litaingia katika udongo mzuri, litaleta matokeo. Daima imekuwa hivyo, Wewe ulisema ingekuwa hivyo, na hivyo ndivyo inavyoenda. Daima imekuwa hivyo.

180 Na, Baba, ninaomba, usiku wa leo, ya kwamba katika kundi hili dogo hapa, kwamba atashuka asilimia mia moja juu ya kila mtu. Jalia wajue ya kwamba kuja kwa Bwana Yesu kumekaribia. Hatujui saa, hakuna ajuaye, ni Baba peke yake tu ajuaye. Yesu alikiri ya kwamba Yeye hakujua. Mungu tu pekee ndiye anayejua ni lini atakapomtuma. Lakini, Bwana, Wewe ulitupa ishara, tunajua ya kwamba ishara hizo zinaonekana. Tunaona kwa Maandiko ya kwamba kuzuriwa kwa mwisho ambako Wayahudi walipata, na sasa kuzuriwa kwa mwisho walikopata Wasamaria, kuzuriwa kwa mwisho ambako Mataifa watapokea, kulikotabiriwa, kulisema, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

181 Ee Mungu, kama ungenipaka mafuta usiku wa leo, kwa Roho wa Kristo, isingefaa kitu isipokuwa Wewe ulitie mafuta Kanisa Lako mafuta vivyo hivyo, inatuhitaji sisi pamoja. Hatujagawanyika, sisi ni mwili mmoja, Bwana. Ninaomba ya kwamba utatujalia. Na jalia, ibada itakapokwisha, jalia kusiwe na mtu mnyonge miongoni mwetu. Jalia hapo, kila mmoja wao, jalia Neno hili liingie mioyoni mwao, na jalia walipokee. Na jalia ishara kuu na maajabu yafanyike.

182 Kama ukitujalia, Bwana, tutaendelea na uponyaji wa Kiungu, kama sivyo, basi tutaendelea tu na wokovu. Mapenzi Yako na yatendeke, Bwana, kuonyesha ya kwamba tunaamini katika Injili yote, na kuamini ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Wewe ni Mungu wa Mbinguni aliyetiwa mafuta, na Wewe ni yeye yule, nasi tunakuamini Wewe kuwa ni yeye yule, kwamba Wewe unaishi milele, daima umeketi kwenye mkono wa kuume wa Ukuu, unayeishi daima kufanya maombezi tunapokiri. Tunaamini hilo, Baba.

183 Tunaomba ya kwamba utatufungia ndani, katika Ufalme wa Mungu sasa, na kujidhihirisha Mwenyewe kwetu. Pia jalia watu wajue ya kwamba hukumu itakapopiga mahali hapa, basi, Bwana, hakutakuwa na udhuru, na ijulikane. Katika Jina la Yesu. Amina.

184 Nimewaweka kirefu, hatutawaita wengi sana, labda tuwachukue wengine kesho usiku. Aliniambia alisambaza kadi za maombi, nafikiri. (Ilikuwa ni nini? A, moja.) A, moja hadi mia moja. Vema. Hatuwezi kuwasimamisha wote kwa wakati mmoja, tunawasimamisha tu tuwezao, wowote tunaoweza kuwasimamisha.

185 Sasa, baadhi yao hapa kwenye viti vya magurudumu na kadhalika. Sasa, itatubidi kuwaita, na ndipo tutakapofanya hivyo, tutahakikisha ya kwamba umeletwa hapa juu, namba yako itakapoitwa. Lakini kama tu. . . Tutawachukua mmoja tu kwa wakati mmoja, kwa sababu kuna walemavu wengi.

186 Sasa, ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja? A, namba moja. Inua mkono wako, yeyote aliye nayo. Kadi ya maombi A, namba moja. A, namba moja. Unaweza kutembea? Vema. A, namba mbili. Ni nani aliye na A, namba mbili? Yule mama. . . Unasemaje? Namba moja? Kuna kasoro. Angalia kadi yake hapo, angalia ni kadi gani aliyo nayo. Huyo mama alielewa vibaya, hana kadi ya maombi. Vema. A, namba moja. Wewe. . . Hebu kidogo, mama, kama huna kadi, si lazima uwe na moja, keti tu hapo na uamini, na uangalie yale Roho Mtakatifu atakayofanya. Unaona? Vema.

187 Ni wangapi wanaojua kuna wengi zaidi wanaoponywa huko nje wasio na kadi za maombi, kuliko walio hapa? Ni wangapi hapa wasio na kadi ya maombi (Inueni mikono yenu.), nawe unajua ya kwamba Mungu anaweza kukuponya? Hebu mwangalieni tu sasa, kwa dakika chache tu, kama akija. A, namba moja. Ni mwanamke yupi aliyekuwa na kadi ya maombi A, namba moja? Vema. Simama. Ni—ni namba moja? Namba mbili, ni nani aliye na namba mbili? Namba tatu. Njoni hapa juu kwa dakika moja, ninyi watatu. . . ninyi wanawake. Namba mbili, moja, mbili. Namba tatu, ni nani aliye na namba tatu? Namba tatu, njoo *hapa*. Nyinyi nyote upande *huu*, kama unaweza kutembea, kama huwezi, vema inua mkono wako, tutakubeba hapa juu. Unaona? Namba moja, mbili, tatu. Nne, ni nani aliye na kadi ya maombi namba nne? Inua mkono wako. Namba nne. Mama huyo papo *hapo*. Njoo papa hapa.

188 Namba tano, namba tano. Vema. Namba sita. Kusanyikeni tu *hapa* upande *huu hapa*. Namba sita. Mabawabu, mtu fulani, ashuke aende kule, Ndugu Roy, baadhi yenu, wasaidieni watu. Vema. Namba sita. Moja, mbili, tatu, nne, tano. Namba sita, ni nani aliye na kadi ya maombi namba sita? Moja, mbili, tatu. Namba sita. Vema, mama, moja kwa moja mstarini. Namba saba. Papa *hapa*. Unaweza kusimama? Loo, sawa. Namba saba. Namba nane. Vema, hapo, mama. Namba tisa. Papa *hapa*, vema, mama. Namba kumi, namba kumi. Kadi ya maombi namba kumi. Ungesemaje katika Kihispania? Je, kuna Wahispania wengi hapa? Namba—namba kumi. Vema, bwana. Namba kumi na moja.

189 Tunawatakeni, kila mmoja aliye na kadi ya maombi, tutawaombea, kwa sababu tuna—tunawajibika kufanya hivyo; wewe shikilia kadi yako. Namba kumi na moja. Ilipata. . .? Namba kumi na mbili. Hilo ni sawa. Sasa, sasa, namba kumi na tatu. Ngoja kidogo, mama huyu *hapa*. Hiyo ndiyo namba yake? Vema. Namba kumi na nne. Vema. Sasa, namba. . . Hiyo ni kumi

na tatu? Kumi na tatu, *hapa*. Sasa, mtu fulani aliinuka kimakosa, mnaona. Hiyo ni kumi na tatu? Kumi na nne. Vema. Hilo ni sawa. Vema.

190 Wanapataje. . .? Walundike kwenye hicho chumba kingine. Sasa, hebu na tungoje, na kuwapitisha hawa, na ndipo tunaweza kuwaingiza wengine tunapowafikia. (Kama utaondoa hiyo, kama inaweza kusogezwa, ama, loo, wanaweza kuizunguka, nadhani, kama ninii . . .) Vema.

191 Sasa, kila mmoja wenu hapa ndani, hakuna mtu ni—nijuavyo mimi, aliye hapa, ninayemjua, isipokuwa huyu awe ni mvulana wa Ndugu Evans, aliyeketi papa *hapa*. Na—naamini huyo ni Ronnie Evans. Hiyo ni kweli, Ronnie? Vema. Huyo ndiye mtu pekee ninayemwona humu jengoni ambaye kwa kweli ni—ninamjua, nje ya Ndugu Borders, meneja, na mwanangu, popote alipoenda, mchungaji hapa; wengine wenu ni wageni.

192 Sasa, naona yapata asilimia tisini yenu ni wagonjwa. Sasa, huko juu kwenye roshani pia, haijalishi uko wapi, kama wewe ni mgonjwa huko juu, huna kadi ya maombi, inua mkono wako, useme, "Mimi ni mgonjwa." Vema. Aminini huko juu. Sasa, kumbukeni, wakati anapowapanga, hebu niwape Andiko lingine, Ninawatakeni muandike Maandiko haya na kuyakumbuka.

193 Sasa, ndugu wahudumu, na *hapa* nje, ni wangapi wanaojua hili, ya kwamba Biblia ilisema kwamba "Yesu ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu"? Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? Vema, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule aliyekuwa jana, angetenda vile vile leo alivyotenda jana. Hiyo ni kweli? Mnaamini hilo, inua mkono wako.

194 Sasa, nitaomba, mkiweza, kama hamtasogea sasa kwa dakika chache. Ketini tu kwa uchaji kwa dakika chache. Msisogee hata kidogo. Na, jamani, wawekeni watoto wenu karibu nanyi mwezavyo sasa, maana hatushughuliki. . . hatuigizi kanisa. Na mara nyingi . . . Ni wangapi wanaojua hawa hutoka kwa mtu mmoja wakamwingia mwingine? Mmeliona likitukia, naam bwana, mara nyingi. Watu wanaketi tu moja kwa moja vitini mwao na kukunjamana, wamepooza; mkawaona wakianguka wakafa moja moja kwenye. . . moja kwa moja kwenye. . . moja kwa moja jukwaani. Hiyo ni kweli. Hatuigizi kanisa, hamna budi kuwa na kicho. Sasa, hili ni takatifu.

195 Sasa, Biblia ilisema ya kwamba "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele," na inasema ya kwamba "Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu," kila mtu anashuhudia ya kwamba hiyo ni kweli. Sasa, ungejuaje kwamba ulimgusa? Wewe. . . Yeye angetenda vile vile alivyotenda alipokuwa hapa. Vema, alifanyaje? Hebu niwape mfano, maana ninawafanya. . . nikijaribu kuwafanya mwamini

ya kwamba Yeye ni yeye yule. Hajabadilika. Biblia, Maandiko yangu, ni kwamba Yeye ni yule yule.

196 Sasa, wakati hiyo...katika...kulikuwako na mwanamke, tuseme hakuwa na kadi ya maombi, bali alitaka kuingia kwenye...aliamini Yeye alikuwa ni Mtu mtakatifu, Nabii, naye akasema, "Nikiweza tu kugusa upindo wa vazi Lake, nitaponywa." Mnaijua hadithi hiyo? Naye akajizongazonga katikati ya umati mpaka akamgusa. Sasa, yeye ka-...Yeye kamwe hakuuhisi kimwili, mwajua, kwa sababu vazi la Kipalestina linapwaya, lina vazi la ndani pia. Lakini kamwe hakuuhisi kimwili, kwa sababu Petro alimkemea, wakati aliposema, "Ni nani aliyenigusa?"

Ndipo Petro akasema, "Bwana, mbona," akamkemea, kasema, "umati wote unakugusa Wewe."

197 Akasema, "Lakini naona kwamba nimekuwa dhaifu, nguvu zimenitoka," ndipo akaangalia pande zote. Mnaona, Yeye alikuwa ameguswa kwa mguso wa namna nyingine. Ndipo akageuka na kuliangalia hilo kusanyiko, mpaka akampata maskini mwanamke yule aliyemgusa, Naye akamwambia juu ya kutokwa kwake na damu na kusema, "Imani yako imekuokoa." Je, huyo alikuwa ni Yesu jana?

198 Vema, kama Yeye ni yeye yule leo, "Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu," hivi Yeye hawezi kukugusa kama utamgusa? Hivi Yeye hawezi kufanya kazi ile ile?

199 Sasa, ninii...Sasa kumbukeni, huenda akatumia sauti yangu, kama ndivyo, mimi ni kama tu maikrofoni hii, ni bubu bila kitu cha kuizungumzia. Sawa. Sikujui, lakini Yeye anakujua. Kwa hiyo huenda ukanigusa, isingefaa kitu, ukiwagusa hawa wachungaji, isingefaa kitu, wao ni watu kama tu nilivyo mimi, lakini ukimgusa Yeye mara moja, angalia litakalotukia. Sasa, si lazima uwe *hapa*, si lazima uwe jukwaani, ninii tu, amini tu.

200 Sasa, hii ni picha ya mahali nilipokuwa nikizungumza usiku wa leo, katika Yohana Mtakatifu mlango wa 4, kama unataka kuisoma utakapofika nyumbani. Huyu hapa mwanamume na mwanamke, simjui mwanamke huyo, sijawahi kumwona maishani mwangu, ni mgeni kabisa kwangu. Muda mfupi uliopita walisambaza kadi za maombi, naye ha-...akapata moja.

201 Yule mvulana huja hapa mbele yenu nyote, anachanganya hizo kadi za maombi ili asijue ni ipi anampa nani, kwa hiyo anawakabidhi tu, chochote mtakacho. Ndipo ikatokea...Nami ninawaita kutoka mahali popote, labda kesho usiku, huenda nikaanzia kwenye sitini na tano, ama arobaini na tano, ama ishirini na tano, ama—ama tisini na kurudi nyuma. Mnajua hilo, mmekuwa mikutanoni.

202 Kwa hiyo ilitokea tu usiku wa leo. Nami ninaona hiyo saa ikizunguka pale, wala sitaki kuwashikilia. Lakini ilitokea tu kwamba mwanamke huyu alifikia mahali nilipoanzia, namba moja. Nadhani wewe ndiwe yule mwanamke, sivyo? Wewe ndiye—wewe ndiye mtu huyo? Vema. Hatufahamiani, hatufahamiani. Hii ni mara yetu ya kwanza kukutana. Hapa kuna mandhari ndogo: Huyu hapa mwanamume na mwanamke, wakikutana kwa mara ya kwanza, kama vile Yesu na yule mwanamke kisimani, watu wawili, ambao hawajawahi kukutana hapo awali, nasi hapa tumesimama.

203 Sasa, kama nilimwambia huyu mwanamke, "Bwana alinituma kuwaombea wagonjwa, nitakuwekea mikono yangu." Huenda ikawa hayuko hapa kwa ajili ya ugonjwa, labda ni tatizo la kinyumbani, labda ni tatizo la kifedha, labda ni kitu kingine. Labda yeye hata si Mkristo, sijui. Lakini kama Yeye anaweza kumwambia yaliyokuwako, kisha amwambie yatakayotukia, hakika angeweza kuamini yale yatakayotukia, kama Yeye anaweza kusema yale yamekuwako. Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaamini hilo sasa? Vema.

204 Sasa, kama mtu yeyote anafikiri kuna kasoro fulani, kwamba una mpango bora zaidi, wazo bora zaidi, umekaribishwa kuja hapa na kuchukua mahali pangu. Usipofanya hivyo, basi tulia kulihusu. Mnaona?

205 Sasa angalieni, sasa, hili hapa, ndiyo kwanza nihubiri Neno ya kwamba Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na kuthibitishwa kwa Maandiko ya kwamba anaishi leo katika Kanisa Lake, naye yuaja, na ile ishara ya mwisho aliyowapa Wayahudi, Wasamaria, na sasa kwa Mataifa.

206 Tumekuwa na . . . Wayahudi walikuwa na miaka elfu nne ya kuamini Nabii anaingia, katika hali Yake kuu, wakati kanisa likiendelea; Mataifa wamekuwa na miaka elfu mbili ya ukanisa, na sasa juu ya . . . kufikia kunena kwa lugha, na uponyaji wa Kiungu, na sasa, moja kwa moja hadi wakati wa mwisho, ambapo Masihi mkuu katika utimilifu wa Roho Wake, akitenda kazi, si katika mtu mmoja tu, katika Kanisa zima, kutiririka.

207 Sasa, haidhuru ningeamini kiasi gani, mwanamke huyu hana budi kuamini pia.

208 Na sasa ninyi huko nje, ambao hamtakuwa kwenye mstari wa maombi, mtazameni Mungu na kusema, "Mungu, maskini jamaa huyo mdogo anayesimama pale hanijui, hajui lolote kunihusu mimi, lakini niko—niko katika hali mahututi, jalia niguse vazi Lako, Nawe ujibu kupitia kwake na kuniambia jambo fulani." Jaribu hilo. Angalia kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Usilijaribu, liamini. Mtu yeyote anaweza kulijaribu. Hatumjaribu Kristo, tunamchukua tu na kumwamini; Yeye haji kwa kujaribu.

Sasa, kama Roho Mtakatifu atafunua. . .Sina budi kuzungumza naye kwa dakika moja.

209 Sasa, angalieni hapa, niko Spokane. Kwa nini nikaja Spokane? Hata tulikuwa na shida kufika hapa, ilitubidi kubadilisha mikutano na nchi nyingine. Nilipaswa kuwa hapa baadaye, lakini ilinibidi nibadilishe. Lakini hata hivyo, nasi. . . Nafikiri wasingeweza kupata jengo, iliwabidi kuja kuchukua kanisa la huyu ndugu, na hawa ndugu wengine, wazuri sana, waliingia, wakishirikiana na huyu ndugu hapa. Hilo ni tamu, la kupendeza; hivyo—hivyo ndivyo ninavyotaka kuona Kanisa likiendelea.

210 Sisi hapa, tumesimama hapa namna hii. Nami huyu hapa. Kwa nini? Mungu alinituma hapa, nilijisikia kuja hapa. Sijali nitapigana vita kiasi gani, Yeye alisema nije hapa, nami huyu hapa. Si kwa sababu sikuwa na mahali pengine pa kwenda, hebu mwulizeni meneja, tuna kitabu cha mialiko, kote ulimwenguni, mamia yake, lakini nilijisikia tu kuja hapa. Kwa nini? Sijui. Labda ataanzisha uamsho, labda mnapokea Ujumbe wenu wa mwisho. Sijui mimi, siwezi kuwaambia. Lakini Yeye alinituma hapa, sijui ni kwa nini. Mimi huyu hapa.

211 Yesu alipanda hadi Samaria. Kwa nini? Hakujua. Mwanamke akatokea, akaanza tu kuzungumza naye, ndipo akapata tatizo lake. Ndipo akakimbia na kumwambia kila mtu, "Huyo ndiye Masihi."

212 Sasa, ewe mama, kama Roho Mtakatifu angenifunulia jambo fulani lililokuleta hapa, ama jambo fulani ambalo umefanya, ama—ama chochote kile, unajua sikujui, na—na kama angelifunua, ungejua ingebidi itoke kwa nguvu fulani za kiroho. Ingebidi ije. . .Mnajua hilo, sivyo, ndugu? Ingebidi ije kwa huyo dada, ninii tu, ingebidi ije kupitia nguvu za kiroho. Mnaamini hilo, huko nje?

213 Basi inategemea kwamba unafikiri kuwa Hicho ni nini. Mafarisayo walisema, "Yeye ni Beelzebuli." Lakini waaminio walisema, "Ni Masihi." Walikuwa watu wa Kimaandiko wanaoamini Maandiko.

Sasa, nitazungumza tu na mwanamke huyu. Na tafadhali mwendelee kuketi. Sasa, msisogee kwa sababu. . .

214 Mnasema, "Ndugu Branham, unasitasita kwa ajili ya jambo fulani." Bila shaka. Je, walikuwa na picha ya yule Malaika hapa juu? Hiyo hapo huko Washington DC, na kadhalika, Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichowahi kuthibitishwa kisayansi. Nguzo ile ile ya Moto niliyowaambia ilikuwa pamoja na Israeli. Wakati ilipofanyika mwili, tunaona kile ilichofanya katika mwili.

215 Sasa, kama hiyo ni Nguzo ile ile ya Moto, itajidhihirisha Yenyewe vivyo hivyo, ni Uzima ule ule. Ukiweka uhai wa zabibu katika tawi la boga, utazaa zabibu. Bila shaka utazaa. Uhai ulio

ndani yake ndio unaozaa tunda. Kristo alisema, "Mimi Ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi." Yeye amepaa juu na kuurudisha Uhai Wake, Uhai Wake unashuhudia.

216 Sasa, kama hiyo ni . . . Ninangojea huo upako, na usipokuja, nitaweka tu mikono juu ya huyu mwanamke, nimwombee, na kuendelea. Sijui, siwezi kusema. Ni kusitasita, ama, ninasitasita, nikiingojea. Hiyo ni kweli kabisa.

217 Kila mtu ana shida gani? Kuna shida gani? Hivi hamwezi kuamini? Amini, rafiki. Huku Maandiko yamewekwa hapa mbele zenu, na hivi mtu aje hapa, na kuthubutu mbele ya kusanyiko la watu kulichukua Neno la Mungu, na kutoa changamoto kwa ulimwengu mzima Kwalo? Amini, kuwa na imani. Amina.

218 Sasa, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ninachukua kila roho hapa ndani chini ya mamlaka ya Roho Mtakatifu, ambaye amenitia upako. Sasa, iweni na imani. Angalieni hapa kwa muda kidogo tu, kama vile Petro na Yohana walivyosema, "Tutazame sisi." Ninatumaini kwa ajili yako. Sijui. Umesimama tu hapa, mwanamke. Lakini kama Roho Mtakatifu atanifunulia jambo fulani lililo maishani mwako, utajua kama ni kweli ama si kweli.

219 Ninazungumza nanyi kibinafsi, hiyo ndiyo sababu nina mtu fulani hapa juu, nipate tu mawasiliano. Roho hunitia upako, na ndipo ni—ninaweza kuliendea kusanyiko, ama popote pale, mnaona, popote Yeye atakaponiongoza basi.

220 Sasa, ninazungumza nanyi tu nipate kujua, nione tu kile Yeye angeniambia. Sijui, hilo lingekuwa juu Yake kusema, bali nina hakika Yeye atafanya hivyo. Naam, bwana. Huyu mama ananiondokea, anaondoka. Angeweza kushuhudia, sasa hivi, kuna hisia inayomzunguka kama hisia tamu sana, nyenyekevu, maana ile Nuru inakaa moja kwa moja juu ya huyu mwanamke. Naye mwanamke huyo anaugua ugonjwa wa koo. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, mama. Unaamini?

221 Ni kwa nini bila kubadilika, kila wakati, mtu fulani atawazia "Alibahatisha hilo"? Nina wazo zuri la kumtaja yule aliyefanya hivyo. Usifanye hivyo. Wewe amini. Sikubahatisha hilo kwa mwanamke huyo, anajua nisingeweza kufanya hivyo. Ingewezaje kuwa kamilifu, na kuwa . . . ?

222 Hapa tu, anaonekana kuwa ni mtu mzuri sana, hebu nizungumze naye kwa dakika moja. Sasa, lolote alilowaambia, nisingejua. Liko kwenye kanda, mnaona. Niko mahali pengine, ni kama kiwango kingine, ni ono. Hivi hamwoni? Naam. Ni ninii . . . ni koo. Una ugonjwa wa koo, pia unasumbuliwa na wasiwasi, unaonekana kuwa na wasiwasi sana. Vema, una magonjwa ya ziada tu, mambo mengi yanayokusumbua, unakuwa mchovu sana, jioni sana, unachoka, unadhoofika, ukimaliza kazi yako. Hiyo ni kweli.

223 Jambo lingine, kuna mtu mwingine unayemjali, unamwombea. Ninaona mtu akitokea. Ni—hapana shaka... hapana shaka ni mume wako. Iko mahali pale pale. Mtu huyo yuko hapa sasa. Unaamini ninaweza kukwambia ni nini, shida ya mume wako? Je, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Mume wako anaugua ugonjwa wa moyo, yeye pia ana wasiwasi. Na—nawe ulimleta mtu fulani kutoka...ni dada yako, ulimleta kutoka kwenye—kwenye nyumba ya uuguzi. Ameketi papa hapa, hiyo ni kweli, amelemaa.

224 Unaamini? Sasa, Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Basi hilo linaleta nini? Kristo hapa pamoja nasi. Unaamini kwa moyo wako wote? Basi nenda ukapokee ulichoomba. Usiwe na shaka. Unaweza kupata ulichoomba, Mungu atakuwa pamoja nawe.

225 Sasa, msisogee huku na huku. Kaeni kimya kabisa, kaeni kimya, kaeni kimyya; wenye kicho. Mnaona, kila mmoja wenu ni roho, na mnaposogea ninaweza tu...unaweza tu kujua, inasonga, kuna kasoro. Mnaona? Iweni tu na kicho kabisa sasa, kimya.

Huyu ndiye huyo mama.

Yule—yule Malaika wa...Nuru ninayoiangalia, ilionekana *hapa* mahali fulani, papa *hapa* ndani. Iweni na kicho kabisa. Sasa, endeleeni tu kuomba.

226 Sasa, kama nikiangalia chini, niseme, "Vema, mtu *huyo*, amelala kwenye machela, amelemaa, ama ana yabisi kavu, anaenda..." Ungesema, "Hakika, iangalieni, hakika ndivyo, mnaweza kuona hilo." Lakini hapa mtu huyu anaonekana wa kawaida kabisa. Ana shida gani? Jambo ndilo hilo. Sasa, angalia huku kwa muda kidogo tu, mama. Hatufahamiani, mara yetu ya kwanza kukutana. Roho Mtakatifu mkuu yupo hapa. Unaamini hilo? Unamhisi. Hiyo si ni Hisia tamu? Unaona, inasikika tu... Nikijua wewe ni Mkristo, kuona ukaribishaji ndani ya Roho huyo, inaonekana tu kana kwamba ni ninii—ninii tu...hiyo ni—hiyo ni, Hisia tamu sana, nyenyekevu. Ni jambo zuri sana kuwa Mkristo.

227 Sasa, kama Bwana Yesu ataniambia tu jambo fulani kukuhusu wewe, ama kile kilichokufanya usimame hapa, kile unachotaka kutoka Kwake, ungeamini kama Yeye angeweza kukwambia i—ilihusu nini.

228 Sasa, kama ningeweza kukuponya, ningefanya hivyo, lakini siwezi, unaona. Kama angekuwa amesimama hapa, amevaa suti hii aliyonipa, asingeweza kukuponya, kwa sababu uponyaji wako tayari umenunuliwa, angekufanya ujue ya kwamba ilikuwa ni Yeye, na jinsi ambavyo angelifanya, kupitia kwangu akijithibitisha Mwenyewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele; yale tu niliyohubiri. Kusanyiko, naamini sote tunaamini hilo. Naam.

229 Sasa, wewe amini tu. Unaugua ngiri. Hiyo ni kweli, ni kweli. Halafu una kasoro upande wako wa kulia. Una maumivu ambayo yanapiga na kushuka chini kabisa upande wako wa kulia, mpaka miguuni mwako. Hiyo ni kweli, sivyo? Unaamini ya kwamba huyo ni Kristo ambaye amekutia mafuta sasa? Mkubali Yeye kama Mponyaji wako, kazi iliyomalizika. Yote yatakuacha, wala hutakuwa nayo tena kama utaamini. Mungu akubariki. Mungu akubariki, dada yangu.

230 Mimi siponyi. Mimi . . . Kama Yeye angekuwa amesimama hapa, asingeweza kuponya. Ni wangapi wanaojua hilo? Tayari amefanya hivyo. Mnaona, anakujulisha tu ya kwamba Yeye yupo hapa, amefufuka katika wafu. Hilo ndilo jambo pekee angaliweza kufanya, kujitambulisha Mwenyewe ya kwamba Yeye angali ni Masihi.

231 U hali gani? Nadhani hatufahamiani. Sijawahi kukuona maishani mwangu, nasi tumesimama tu hapa kwa mara ya kwanza, mwanamume na mwanamke wakikutana.

232 Kuna mwanaume anayeendelea kuja mbele zangu, mnaona, ni mtu fulani anayeomba. Wewe endelea tu kuomba, hilo ni sawa. Hiyo ni kweli. Wewe mguse tu. Ninawaomba tu, katika Jina la Bwana Yesu, kuamini yale niliyosema kwamba ni kweli, kwa kuwa nimesema kweli, nanyi mnajua hilo ni kweli, linatoka kwenye Neno. Na kama nimesema kweli, Mungu anawajibika kwa Neno Lake Mwenyewe. Mnaona? Hawajibiki kwangu, Yeye anawajibika kwa Neno Lake. Mnaona? Ninanena tu Neno Lake.

233 Sasa, bila kukujua, lakini kama Bwana Yesu angeniambia jambo fulani kukuhusu wewe, ama jambo fulani ambalo umefanya, ama jambo fulani ambalo hukupaswa kufanya, ama baadhi ya . . . shida uliyo nayo, na labda ni ya kifedha, ya kinyumbani, sijui. Lakini kama atalielezea tu, utajua ya kwamba hapana budi kuwe na namna fulani ya nguvu. Itabidi liwe ni Neno la Mungu, kwa sababu "Huyatambua mawazo ya moyo." Hiyo ni kweli. Unaamini ya kwamba Mungu aliituma hii, katika siku za mwisho, na ni Kristo akishuhudia kuja Kwake hivi karibuni? Kama unaamini hilo, basi Mungu hakika atakujalia haja yako.

234 Una henia, mbili. Hiyo ni kweli. Una tatizo lingine, ambalo ni ugonjwa wa kibofu. Hiyo ni kweli, sivyo? Unaamini Yeye anajua wewe ni nani? Bibi Peterson. Huyo ndiye uliye. Sasa, nenda ukiamini na, haitakusumbua tena. Amini. Usiwe na shaka. Unaamini? Mwamini tu Mungu. Usitie shaka. Usitie shaka.

235 Hatufahamiani, lakini Bwana Yesu anatujua sote wawili. Na unafikiri ya kwamba Yeye angeweza kufanya jambo fulani, ama kuniambia jambo fulani kukuhusu ambalo lingekusaidia? Ungeamini?

Sasa, mnatambua hali iliyonipata sasa hivi, ninatetemeka tu mwili mzima. Unasema, "Mbona, Ndugu Branham? Kwa nini ufanye hivyo?"

236 Vema, kama maskini mwanamke mmoja, akigusa upindo wa vazi la Yesu, alimfanya Mwana wa Mungu dhaifu, unafikiri ingenifanyia nini, mwenye dhambi, aliyeokolewa kwa imani? Hii hapa njia pekee ningeweza kufanya hata moja ni kwa sababu Yeye alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya; nyingi kuliko hizi mtazifanya."

237 King James inasema "kubwa zaidi," bali halijafasiriwa vizuri, tafsiri sahihi ni "nyingi zaidi." Ni nani angeweza kufanya makubwa zaidi? Aliwaponya wagonjwa, akawafufua wafu, akasimamisha maumbile, Alifanya kila kitu kilichokuwepo kufanywa. Mnaona? Unafanya tu mengi zaidi ya hayo, kwa sababu Yeye angegawanyika miongoni mwa Kanisa Lake, "nyingi kuliko hizi."

238 Sasa, huyu hapa maskini msichana aliye mdogo sana wa umri kuniliko mimi. Simjui, sijawahi kukutana naye. Hatufahamiani, lakini Roho Mtakatifu anatujua sote wawili. Na kama Roho Mtakatifu atanifunulia kitu kama hicho, je, italifanya kusanyiko lote kuamini? Kila mtu?

239 Huu *hapa* mkono wangu, hii *hapa* Biblia, simjui mwanamke huyu. Mnaona? Naye huyo hapo amesimama. Huenda alikuwa mkutanoni mahali fulani. Uliwahi kuwa katika mmoja wa mikutano yangu hapo kabla? Hajawahi kuwa mkutanoni, hata, hapo awali. Amesimama tu hapa. Kabisa hatufahamiani.

240 Vema. Roho Mtakatifu na akujalie haja yako, Dada. Naam. Mama huyo anaugua ugonjwa wa rektamu. Ana ugonjwa wa uvimbe wa utumbo mpana, ambao umesababisha jambo hili. Umekuwa na shida nyingi sana maishani mwako, sivyo? Ninakuona ukienda hospitalini, la, moja, mbili, tatu, nne, tano, mara sita, upasuaji. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Amini kwa moyo wako wote, na yote yamekwisha.

Unaamini?

241 Njoo hapa. Unaamini Mungu anaweza kuponya ugonjwa wa moyo? Vema. Endelea, ondoka jukwaani.

242 Unaamini? *Hapa*, ukiinua mkono wako, unaamini Yeye huponya huo ugonjwa wa tezi dume ulio nao, akupe afya? Vema, kama unauamini, unaweza kuwa nao pia, kuwa tu na imani.

243 U hali gani, mama? Unaamini Yeye huponya yabisi kavu? Vema, endelea tu kutembea basi, Naye atakufanya mzima, ninii tu, atakuponya, ikiwa utaamini.

244 Na wewe je, mama? Ungetaka kuuondokea ugonjwa huo wa tumbo na uwe mzima? Endelea tu kutembea, ukisema, "Asante, Bwana. Ni—ninaupokea."

Kama unaweza kuamini! Ni nini...? "Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio."

245 Unaamini? Vipi kama sikukwambia kitu, nilikuwewekea tu mikono? Ungeamini? Unaamini ungepona? Njoo hapa. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

Huyo ni yule ambaye hakutaka kuona chochote. Mnaona? Aliamini tu kwamba chochote kile, ilikuwa sawa.

246 Njoo, mama. Vipi kama sikukwambia chochote? Ungeamini jambo lile lile? Vema, ukiamini, hiyo shida ya kike... Nimekwisha kukwambia, kwa hiyo endelea. Shida hiyo ya kike...?...itaondoka na kukuacha, nawe utakuwa mzima, ikiwa tu utaamini kwa moyo wako wote. Amini.

247 Unaamini kwa moyo wako wote? Nenda ukale chakula chako cha jioni na kusema, "Asante Bwana kwa kuniponya." Amina. Mungu akubariki. Kuwa tu na imani. Usitie shaka. Amini tu kwa moyo wako wote.

248 Njoo, mama. Umekuwa na tumbo lenye fadhaa kwa muda mrefu. Lilikutatiza sana. Limekwisha sasa. Unaamini? Vema, nenda zako, ukisema, "Asante, Bwana."

Ni wangapi wanaoamini huko nje, kwa moyo wako wote? Mnaamini ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu? Yeye yule jana, leo, na hata milele?

Unaamini? Anza kuondoka jukwaani basi, ukisema, "Asante, Bwana."

Kuna Kitu fulani kilichonipa upako, sivyo? Ninakuwekea mikono, nikisema, "Bwana asifiwe." Upako fulani.

Njoo. Unaamini? Kuwa na imani. Katika Jina la Bwana Yesu, nenda ukaponywe, amini.

249 Njoo. Nisipokwambia chochote, utaamini hata hivyo? Vema, una wasiwasi. Vema, unaninii...umekuwa na wasiwasi kwa muda mrefu. Kwa kweli, jambo moja ni hilo badiliko, kule kukoma hedhi ambako kumekuvuruga kabisa. Unapata vipindi vya huzuni sana, nawe...kila mtu anasema, "Jirudie," lakini huwezi, kuna kitu kinachokutisha. Lakini kimetoweka sasa, hakitarudi. Unaona? Liamini tu kwa moyo wako wote. Nenda zako ukaamini kwa moyo wako wote.

250 Unaamini? Mtu fulani huko nje kwenye kusanyiko aamini. Loo! Unaamini? "Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Mnajua haiwezi kuwa ni mimi. Vema, mnafikiri ni Nani?

251 Vipi kuhusu maskini mwanamke huyu wa Kimeksiko, aliyeketi hapa? Anasumbuliwa na vipindi vya kizunguzungu. Hiyo ni kweli. Unaamini? Ulimgusa nani? Ulimgusa Kuhani Mkuu. Kamwe hukunigusa mimi, uko mbali sana nami. Vema, vipindi vyako vya kizunguzungu vimekuacha. Amina. Amina.

Mwulize kama hiyo ni kweli. Hmm. Mwaminini tu Mungu, mwaminini Mungu.

252 Na wewe je, uliyelala hapo kwenye machela? Naam, wewe. Unaamini kwa moyo wako wote? Ulielekeza kidole chako. Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu, ama, mtumishi Wake? Nitasema hivyo, hilo huwakwaza watu. Unaamini? Kama. . .Siwezi kukuponya, bwana, lakini Mungu anaweza. Kama ukilala hapo, utakufa. Madaktari hawawezi kukufaa kwa chochote. Jambo moja, una ugonjwa wa tumbo, una yabisi kavu mgongoni mwako, bali hakuna mtu anayeweza kuuponya huo ila Mungu. Lakini kama utamwamini Mungu, na kutenda kulingana na Neno, unaweza kusimama, uchukue kitanda chako, uende nyumbani.

Vipi kukuhusu wewe katika machela hiyo nyingine, hapo? Unaamini?

253 Huyo hapo anaondoka. Mungu asifiwe. Mnamwona akinyooka? Huyo hapo anaenda. Hebu tumsifu Mungu. Amina. Mnamwamini Yeye? Amina. Yeye si ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Siwezi kuponya, siwezi kuwapa afya, Kristo anaweza.

254 Unaogopa nini? Niliposema, dakika chache zilizopita, kuhusu mwanamke huyo kuwa na wasiwasi, ulinigeuza moja kwa moja. Unahofu. Hakuna kitakachokupata, utakuwa mzima. Unaamini hilo? Ungewezaje kuivuta imani ya Mungu? Ulimgusa nani kufanya nijue ulikuwa ukisumbuliwa na wasiwasi? Unamwamini Mungu? Unamwamini Yeye, unaamini Neno Lake? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Basi katika Jina la Yesu Kristo, simama utoke kwenye hiyo machela, uende nyumbani, na usahau jambo hilo. Unaamini? Toka nje. Simama. Chukua ulicho nacho, nenda nyumbani, ukawe mzima.

Mwaminini Mungu. Mnaamini?

255 Laiti angeamini! Ulikuwa unaomba. Kuna Nuru juu yako. Kama unaamini, utapona hiyo polio na upate afya, urudi kwenye huduma za umishenari. Usitilie shaka.

256 Unamwamini Yeye? Vipi kukuhusu wewe *hapo*? Ugonjwa wa mgongo, ugonjwa wa kibofu, magonjwa ya ziada, yote hayawezi kuninii. . .Hakuna kitu kinachoweza kukusaidia. Kristo, Ndiye pekee awezaye kukuponya. Hiyo ni kweli? Kwa nini usimwamini? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Je, waweza kuchukua neno langu kama Lake, kukwambia Yeye ni yule yule jana na hata milele? Anawezaje kusimama hapa na kukwambia yote kukuhusu wewe mwenyewe, bila ya wewe kuwa na mawasiliano Naye? Kwa nini usimwamini, simama, chukua kitanda chako, uende zako nyumbani, upate afya! Utalikubali, na utoke kwenye kitanda hicho cha wagonjwa.

Mwaminini Bwana Yesu Kristo. Mnayo imani, aminini.

257 Maskini mama huyu aliyeketi *hapa* kwenye kiti *hiki* cha magurudumu, siwezi kukuponya, lakini kama utaamini kwa moyo wako wote, kisukari hicho kitakuacha, nawe utaenda nyumbani, uwe mzima. Mwamini Mungu, amini, ondoka, nenda nyumbani, ukaponywe.

258 Vipi kuhusu wewe uliyelala *hapo*, ukisumbuliwa na kuvuja damu kooni, kila kitu? Unaamini kwa moyo wako wote? Kama unaamini kwa moyo wako wote! Kila kitu ni kibaya kwako, lakini kwa nini usiinuke, na utoke kwenye kitanda hicho, utoke kwenye kitanda hicho cha wagonjwa! Katika Jina la Yesu Kristo, simama! Amina.

259 Hao hapo! Kila mtu anayeamini, mnaamini? "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Mnaamini hilo? Wekeaneni mikono nyinyi kwa nyinyi basi, upesi sana, wekeaneni mikono, kila mwaminio. Hivi hapa, hivi hapa viti vya magurudumu vikiwa tupu, vitanda vya wagonjwa. Wekeaneni mikono na kuomba.

260 Baba wa Mbinguni, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, Shetani na apoteze nguvu zake miongoni mwa watu hawa wakati anapoweza kuwaona viwete, yabisi kavu, waliopindika wanaweza kuja huku na kuponywa. Jalia, Bwana, kwamba wataamini. Katika Jina la Yesu Shetani na awaache. Amina.

261 Kila mtu anayemwamini Yeye, anamkubali sasa kama Mponyaji wako, simama kwa miguu yako, katika Jina la Yesu Kristo na upate afya. Amina. Haya basi: Kila mmoja wao amesimama.

262 Hebu na tumwimbie sifa. Inueni mikono yenu na mumpe sifa. "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Yeye hashindwi kamwe, Yeye ni Mwana wa Mungu, wa Milele, wala hawezi kushindwa kamwe. Mwamini Yeye kwa moyo wako wote, uponywe. Simama uende nyumbani.

62-0712 Sisi Tunataka Kumwona Yesu
Open Bible Standard Church
Spokane, Washington Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org